# Nipashe

Jumamosi Aprili 27, 2024 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-


ISSN 0856 • Na. 0581659

www.ippmedia.com MWANGA WA JAMII

The Guardian digital nipasheTZ nipasheTZ nipasheTZ 0745 700710 LIKE & FOLLOW US




**PPRA,** ZPPDA zatia saini ili kuenzi Muungano UKURASA 4



**Wakili:** Tatizo afya ya akili ni maumivu, mzigo mzito UKURASA 15




**TAKUKURU** yabaini rushwa ujenzi wa ofisi Jiji la Arusha UKURASA 15



**ALBAM YA ZUCHU HIYOO...** UKURASA 12

# Rais Samia ataja mambo matatu kuenzi Muungano

• **Viongozi** Afrika wasema umejenga uchumi... *Endelea Ukurasa 2*



Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Samia Suluhu Hassan akiwapungia mkono wananchi, alipowasili katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana, wakati wa sherehe za Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar. **Picha zaidi Uk. 2&7 PICHA: IKULU**

## Polisi wamsaka aliyesambaza video ya kumdhalilisha waziri UK.3

## YALIYOMO

UKURASA WA 3

### KAMATI YAFANYA UCHAMBUZI WA MIFUMO YA KODI

SERIKALI kupitia Kamati ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi, inaendelea kufanya uchambuzi na tathmini ya mifumo ya kodi, ada na tozo za huduma kwa lengo la kuondoa urasimu na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

UKURASA WA 8

### WAZIRI ATAKA KUIMARISHWA KLABU ZA KIDIJITALI SHULENI

NAIBU Waziri wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhandisi Maryprisca Mahundi amewahimiza wakuu wa shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vikuu kuanzisha klabu za kidijiti shuleni.

## Watoto watatu wafariki dunia kwa kuangukiwa na nyumba usiku

UKURASA 3

**MICHEZO** YANGA HASIRA ZOTE KWA COASTAL LEO UK.24

**MAONI,** UK.6



Baadhi ya wakuu wa vyombo vya ulinzi na usalama wakiwa katika sherehe ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. **PICHA: OMR**

# Samia ataja mambo matatu kuenzi Muungano

**Na Romana Mallya**

RAIS Samia Suluhu Hassan, ametaja mambo matatu makubwa katika kuenzi Muungano ikiwamo kutekeleza falsafa ya maridhiano, kustahimiliana, kuleta mageuzi na kujenga nchi, maarufu kama 4R.

Pia amewataka watanzania kujivunia miaka 60 ya Muungano kwa kuwa wamefanikiwa kuutunza na kuilinda nchi kwa kudumisha amani na utulivu.

Rais Samia aliyasema hayo jana katika sherehe za maadhimisho ya Miaka 60 ya Muungano zilizofanyika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, zikibebwa na kaulimbiu isemayo: "Tumeshikamana, Tumeimarika kwa Maendeleo ya Taifa Letu."

Sherehe hizo pia zilihudhuriwa na marais wa Kenya, Somalia , Burundi, Comoro, Jamhuri ya Kidemokrasia ya Congo (DRC), Zambia na Namibia. Pia ilihudhuriwa na Makamu wa Rais kutoka Malawi na Uganda, Waziri Mkuu wa Msumbiji, Waziri wa Mambo ya Nje wa Rwanda na mwakilishi wa marais kutoka Zimbabwe.

Akizungumza na Watanzania, Rais Samia alitaja mambo matatu makubwa, moja akiwataka watanzania kujivunia muungano huo.

"Ninataka kuwaambia Watanzania tuna kila sababu ya kujivunia Muungano wetu. Nchi ya Tanzania imetokana na maamuzi (uamuzi) yetu (wetu) wenyewe.

"Katika kipindi chote cha miaka 60, taifa la Tanzania likiwa na watu na makabila 120 na linalounganishwa na lugha moja ya Kiswahili, wameimarisha Muungano na mshikamano.Tumeweza kuitunza na kuilinda nchi yetu kwa kudumisha amani na utulivu. Kupitia Muungano tumejenga umoja na mshikamano wa kitaifa.

"Tumeboresha udugu na bila shaka tumepiga hatua kubwa ya maendeleo kiuchumi, kisiasa na kijamii pamoja na kudumisha mila na desturi. Tuna kila sababu ya kujivunia Muungano", alisema.

Jambo la pili, Rais Samia aliwasihi Watanzania katika kuuendeleza Muungano, kutekeleza falsafa ya maridhiano, kustahimiliana, kuleta mageuzi na kujenga nchi. Alisema hayo ndiyo yatakayoendelea kuwajengea amani na utulivu wa kudumu nchini na kuleta maendeleo endelevu. "Leo hii tuna fahari kuwa nchi yetu imefika hadhi ya uchumi wa kati ngazi ya chini, na tathmini zote zinaonesha kuwa, kuna mwelekeo mzuri wa kuimarika na kufikia uchumi wa kati ngazi za juu, hivyo tuendelee kudumisha amani ya nchi yetu ili tujenge uchumi na kuleta ustawi zaidi wa wananchi," alisema.

Rais Samia alitaja jambo lingine akiwataka Watanzania kuendelea kufanya kazi kwa bidii na maarifa zaidi ili wakuze tija na ustawi wa taifa, akikumbusha kauli isemayo 'kazi ndicho kipimo cha utu'. Alisema wanaposimama kutetea haki za Watanzania, hawana budi kutimiza wajibu ambao ni kufanya kazi kwa bidii ili kuwezesha haki za msingi zipatikane kwa maisha ya mwanadamu na kustawisha utu wa watu.

"Niwapongeze Watanzania kwa kutimiza miaka 60 ya Muungano hakika tumeshikamana na tumeimarika. Ninawashukuru wageni wetu kwa kuunga nasi katika maadhimisho haya, hii inamaanisha kwamba nchi yetu imejenga vyema uhusiano wa kidiplomasia," alisema.

### NDOTO CDF MWANAMKE

Katika sherehe hizo, Rais Samia alisema wameona tofauti ya Jeshi la Muungano na jeshi la tarabushi yalivyoonyesha maonyesho mbalimbali, huku akisifu kikosi cha bendera ambacho safari hii kina mwanamke.

"Na huu ndio mwanzo wa safari. Msije mkashangaa mwaka 2030 tuna CDF (Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi) mwanamke hapa. Tulikuwa hatuwezi zile hustle (kupitia shida) za tarabushi lakini kwa maendeleo ya vikosi vya ulinzi sasa, tutakwenda bega kwa bega," aliahidi.

### MAUA KWA WAASISI

"Ninawashukuru kwa dhati waasisi Muungano huu, Mwalimu Julius Nyerere na Sheikh Abeid Amani Karume pamoja na viongozi waliofuata kwa kutuleta pamoja na kujenga taifa huru na madhubuti na lenye matumaini.

"Zawadi pekee tunayoweza kuwapa ni kuendelea kudumisha muungano huu na kuenzi maono yao. Kwa msemo wa siku hizi tunasema, 'tuwape maua yao'," alisema.

Rais Samia alisema wamepata heshima na kuungwa mkono na wakuu wa nchi na serikali ya ukanda wa Jumuiya ya Maendeleo ya Kusini mwa Afrika (SADC) na Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na viongozi waliowakilisha marais wao na pamoja na wadau wa maendeleo.

### MVUA

Katika sherehe hizo, Rais Samia alimtambulisha mdau wa maendeleo kutoka Benki ya Maendeleo ya Afrika ambaye yupo hapo kwa shughuli maalum na kumueleza kuwa, mvua imeharibu barabara na fedha zitatoka.

Rais Samia alisema anatambua wanaoathiriwa na mvua na kuwahakikisha kuwa serikali inafanya kila linalowezekana kurejesha miundombinu iliyoharibiwa.

Pia aliwataka wananchi kufuatilia taarifa za Mamlaka ya Hali ya Hewa (TMA) na kutoa pole kwa nchi jirani zilizokumbwa na maafa ya mvua hiyo.

Hata hivyo, Rais Samia alisema hali ya hewa ya mvua iliyonyesha jana haikuwezekana wote kuwapo uwanjani hapo, akiamini watanzania walikuwa wakifuatilia kupitia vyombo vya habari.

### ILIVYOKUWA

Miongoni mwa mambo yaliyofanyika uwanjani hapo na kuwa kivutio ni onyesho la kwata la askari wa zamani wajulikanao kama askari tarabushi kutoka Jeshi la Polisi ambalo wakati wote amri zikitolewa kutokana na changamoto ya lugha ya Kiingereza, walikosea.

Kwa mujibu wa Sajenti wa Polisi, Suleman Mwaimu, kikundi hicho kilipata umaarufu Zanzibar kabla ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa kuitwa askari wa tarabushi kwa kivazi cha kofia kinachoitwa tarabushi.

Amri zote katika gwaride hilo zinatolewa kwa lugha ya Kiingereza hali iliyosababisha askari kucheza kwa hofu na wasiwasi mkubwa na wakati mwingine kukosea kutokana na kutoelewa lugha.

Historia hiyo inakwenda tangu utawala wa sultan ambapo pamoja na kutawala Zanzibar mambo yote ya kiulinzi yalikuwa chini ya koloni la Uingereza.

# Viongozi Afrika wasema umejenga uchumi

**Na Romana Mallya**

MARAIS na viongozi kutoka Jumuiya ya Afrika Mashariki (EAC) na Umoja wa Afrika (AU) wamesema dhamira ya waasisi wa Muungano unaotimiza miaka 60 hivi sasa, imechangia kuunganisha nchi na kujenga misingi ya kiuchumi na kijamii.

Wakitoa salamu zao jana kwa niaba ya marais wa umoja huo wakati wa maadhimisho ya miaka 60 ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, sherehe zilizofanyika uwanja wa Uhuru mkoani Dar es Salaam, Rais wa Visiwa vya Comoro, Azali Assouman na Rais wa Burundi, Evariste Ndayishimiye, walipongeza hatua iliyofikiwa.

Rais Assouman ambaye amemaliza muda wake wa uongozi AU, akitoa salamu kwa niaba ya umoja huo, alisema; "Ni furaha kubwa kuona ndoto na dhamira za waasisi walioungnisha nchi iliyojenga misingi ya kiuchumi na kijamii."

Alisema Tanzania ni nchi wanayoyopakana nayo na ya mfano kwa amani, demokrasia na maendeleo.

"Tanzania imekuwa mwenyeji wa vuguvugu mbalimbali za kutafuta amani kwa nchi zetu barani Afrika ikiwamo nchi yangu na chama chetu.

"Sitaweza kuondoka hapa bila kuzungumzia udugu na ushirikiano kati yetu. Viongozi waliotutangulia wamejenga misingi ya kukaribisha nchi zetu kuwa na ushirikiano wa karibu, heshima kati ya nchi moja na nyingine na kutakiana mema kimaendeleo kati ya nchi zetu mbili," alisema na kuahidi kuendelea kudumisha ushirikiano na ukaribu uliopo kati ya viongozi na wananchi kwa maslahi mapana ya mataifa hayo.

Rais wa Burundi, Ndayishimiye, akitoa salamu kwa niaba ya viongozi wa EAC, alisema: "Kuna sababu kubwa iliyonitoa Burundi kuja na mke wangu katika sherehe hii. Kabla ya wakoloni kufika kwetu, Waha, Wahangaza na Warundi walikuwa ndugu, walitembeleana."

Alisema Warundi walikuwa wakienda Tanzania kuuza majembe na Waha walikwenda Burundi kuuza chumvi, hivyo si rahisi kuwatofautisha.

"Mkoloni ametutawala sote. Wakati Baba wa Taifa Mwalimu Julius Nyerere akipigania uhuru, vivyo hivyo na mwana Mfalme walikwenda bega kwa bega na kupigania sambamba na kupata ushindi kwa pamoja, furaha ya watanzania ni furaha ya waburundi tupo kama mti na ganda," alisema.

Rais Samia Suluhu Hassan, alisema Rais wa Kenya, William Ruto amemnong'oneza waluo na wamasai wa hapa na Kenya wapo sawa hawawezi kuwatofautisha, vivyo hivyo kwa Rais Zambia, Hakainde Hichilema, hawawezi kutofautisha wakifika mpaka wa Tanzania na nchi hiyo.

Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Ali Mwinyi, alisema mambo mengi yaliyoangaliwa kama changamoto za Muungano yamepatiwa ufumbuzi na machache yapo katika hatua mbalimbali.

"Kwa niaba ya wananchi Zanzibar tunawaahidi watanzania wenzetu tutaendelea kuwa waumini wa Muungano kwa kuhakikisha unadumu na kuimarika kwa kizazi kitakachokuja baada yetu. Ninapongeza sekta zote kwa maendeleo iliyopata kwa miaka 60 ya Muungano," alisema.




Daladala linalofanya safari zake kati ya Mbagala na Mbezi, jijini Dar es Salaam likiwa limetumbukia kwenye mtaro wa maji ya mvua baada ya dereva kushindwa kulimudu katika eneo la Sokota, Manispaa ya Temeke jana na kusababisha majeruhi. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# Polisi wamsaka aliyesambaza video kumdhalilisha waziri

**Na Julieth Mkireri,** KIBAHA

JESHI la Polisi Mkoa wa Pwani linamsaka mtu aliyerekodi video iliyokuwa ikimwonyesha Waziri na Mbunge Mstaafu wa Bagamoyo, Dk. Shukuru Kawambwa, akidhalilishwa kwa maneno, vitisho, dharau na kutishiwa kufungwa pingu.

Kamanda wa Polisi Mkoa wa Pwani, Kamishna Msaidizi Mwandamizi (SACP) Pius Lutumo, alisema jana katika taarifa yake kwamba mtu huyo anayetuhumiwa kusambaza video hiyo ikimwonyesha Dk. Kawambwa na mwenzake Cathbert Enock kwenye mitandao ya kijamii, ajisalimishe katika kituo cha polisi Bagamoyo.

Katika taarifa hiyo aliyoitoa kwa waandishi wa habari mjini hapa, alisema tukio hilo lilitokea Aprili 24, mwaka huu, majira ya saa 8:00 mchana katika kijiji cha Kitopeni wilayani Bagamoyo.

SACP Lutumo alisema mtuhumiwa huyo alisambaza video hiyo iliyokuwa na maneno ya kumdhalilisha Dk. Kawambwa kwamba: "Shukuru Kawambwa Waziri wa Miundombinu enzi hizo, sasa dalali wa viwanja Bagamoyo na mhalifu wa kawaida'.

Alisema katika tukio hilo, Diwani Mstaafu wa Kiromo, wilayani Bagamoyo, Hassan Usinga, na askari mgambo, Abdallah Mgeni, waliwashambulia Dk. Kawambwa na wenzake kwa maneno huku wakilazimisha wafungwe pingu.

Chanzo cha tukio hilo kinaelezwa kuwa ni magari ya mchanga ya mtuhumiwa kuharibu barabara na mashamba ya watu yakipita katika eneo hilo hali iliyosababisha wananchi kufunga barabara kwa magogo kuzuia uharibifu kuendelea.

Kamanda Lutumo alisema watuhumiwa hao wawili, Usinga na Mgeni, walikamatwa na polisi na baadae kuachiwa kwa dhamana kwa mujibu wa sheria na watafikishwa mahakamani uchunguzi ukikamilika kuhusiana na tukio hilo.

Mbali ya tukio hilo kuelezea kutokea Aprili 24, mapema Aprili 25, video ya tukio hilo ilisambaa katika mitandao mbalimbali ya kijamii ikimwonyesha mtuhumiwa akimtolea maneno makali na ya dharau Dk. Kawambwa.

## Kamati yafanya uchambuzi wa mifumo ya kodi

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

SERIKALI kupitia Kamati ya Maboresho ya Mfumo wa Kodi, inaendelea kufanya uchambuzi na tathmini ya mifumo ya kodi, ada na tozo za huduma kwa lengo la kuondoa urasimu na kuboresha mazingira ya biashara na uwekezaji nchini.

Naibu Waziri wa Fedha, Hamad Hassan Chande, alisema hayo juzi bungeni alipokuwa akijibu swali la Mbunge wa Viti Maalum (CCM), Fakharia Shomar Khamis.

Katika swali lake, mbunge huyo alihoji kwa nini kodi ya jengo na kodi ya ardhi zisiunganishwe na kuwa moja ili kumwondolea usumbufu mwananchi.

Akijibu swali hilo, Naibu Waziri Chande alisema tathmini hiyo inajumuisha mapendekezo ya maboresho ya mfumo wa usimamizi wa kodi ya jengo na kodi ya ardhi kama inavyopendekezwa na mbunge huyo.

Sambamba na hatua hiyo, alisema serikali inaandaa mfumo wa kielektroniki wa kutoa ankara ya pamoja kwa huduma zinazolandana ili kuondoa usumbufu kwa wananchi wanaostahili kulipa kodi ya jengo na kodi ya ardhi.

Katika swali la nyongeza, Mbunge wa Mwera (CCM), Zahor Mohamed Haji, alisema kwa kuwa suala la utafiti linahitaji muda, hivyo serikali iwaambie wananchi lini itakamilisha kazi hiyo. "Mifumo ni jambo kubwa na je, serikali iko tayari kuendelea kutoa elimu zaidi kwa wadau?"alihoji.

Akijibu swali hilo, Chande alisema tathmini hiyo ni sehemu ya maandalizi ya muswada wa sheria ya fedha ya mwaka 2024 ambao utawasilishwa bungeni katika mkutano huu wa bunge.

Alisema serikali kupitia taasisi zake zimekuwa zikitoa mafunzo kwa wadau siku kwa siku kulingana na mahitaji.

# Wafariki dunia kwa kuangukiwa na nyumba

**Na Marco Maduhu,** SHINYANGA

WATOTO watatu wa familia moja katika kijiji cha Mishepo wilayani Shinyanga, wamefariki dunia kwa kuangukiwa na nyumba kutokana na mvua inayoendelea kunyesha maeneo mbalimbali nchini.

Taarifa zinabainisha kuwa tukio hilo limetokea usiku wa kuamkia jana majira ya saa 9:00 alfajiri.

Watoto waliofariki dunia ni Nkamba Ngassa (13), Salamu Ngassa (8) na Gigwa Ngassa (6) na kwamba mtoto mmoja na mama yao walinusurika kifo.

Akisimulia tukio hilo, jirani wa familia hiyo, Flora Abdallah, alisema nyumba yao tangu awali ilikuwa imeanguka ukuta mmoja lakini walikuwa wakiishi hivyo hivyo.

Alisema usiku wa kuamkia jana, mvua kubwa ilinyesha kijijini hapo na katika nyumba hiyo, walikuwa wamelala watoto wanne pamoja na mama yao, ndipo nyumba ikaanguka na kuwafukia kasoro mtoto mmoja huku mama yao ikababakizwa miguu tu.

Alisimulia kwamba yule mtoto ambaye alisalia, aliamka na kuona miguu ya Mama yake ndipo akamfukua, na kuanza kutafuta msaada kwa majirani, ili kuwafukua watoto wake watatu.

Mama wa watoto hao, Kashinje Nchembi, alisema mvua ilianza kunyesha majira ya saa 4:00 usiku na ilipofika saa 9:00 alfajiri, nyumba ilianguka na kuwafunika hatimaye kusababisha watoto watatu kufariki dunia.

"Mimi nilikuwa nimefunikwa na kubakiza miguu tu, bahati nzuri mtoto wangu mmoja yeye alibahatika na kuja kunifukua, ndipo nikaomba msaada kwa majirani kuja kuwafukua watoto wangu wengine watatu," alisema Kashinje.

Mwenyekiti wa Kijiji cha Mishepo, Pastory Jackobo, alisema walipofika eneo hilo la tukio majira ya saa 10:00 alfajiri na kuanza kuwafukua watoto hao watatu, waliwakuta tayari wameshapoteza maisha.

Diwani wa Mwantini, Mpemba Jilungu, alisema tayari taratibu za mazishi juu ya watoto hao zinafanyika huku akitoa wito kwa wananchi ambao wanaishi kwenye maeneo hatarishi, ni vyema wakahama, hasa katika kipindi hiki cha mvua nyingi ili kunusuru maisha yao.

Kaimu Kamanda wa Polisi Mkoa wa Shinyanga, Kennedy Mgani, alithibitisha kutokea kwa tukio hilo na kubainisha kwamba tayari wameshaikabidhi miili ya marehemu kwenye familia kwa ajili ya mazishi.

HABARI KITAIFA

# PPRA, ZPPDA zatia saini kuenzi Muungano

**Na Mwandishi Wetu,** DODOMA

WAKATI Tanzania ikisherehekea miaka 60 ya Muungano, Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA) na Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA) zimetia saini rasimu ya mkataba wa maelewano kufanya kazi pamoja na kuimarisha muungano.

Makubaliano hayo yalitiwa saini jana jijini Dodoma mbele ya wenyeviti wa bodi za wakurugenzi za mamlaka hizo, wawakilishi wa wafanyakazi na Makamu Mwenyekiti wa ZPPDA, wajumbe wa bodi zote mbili, Mkurugenzi Mkuu PPRA, Eliakim Maswi na Mkurugenzi Mtendaji ZPPDA, Othman Juma Othman na menejimenti ya PPRA.

Akizungumza baada ya kutia saini makubaliano hayo, Maswi alisema wamekubaliana kushirikiana katika kujenga uzoefu kwa watendaji na kukuza maarifa ya kiutendaji kwa kubadilishana utaalamu katika kutekeleza mbinu za kimkakati na taaluma ya ununuzi.

Pia alisema watashirikiana katika kuzitambua sheria na miongozo ili kuleta tija na uwajibikaji ndani ya taasissi hizo, kuelimishana taarifa na ujuzi muhimu unaohusu ununuzi wa umma na uendeshaji mali za umma, kuhabarishana, kubadilishana uzoefu na kuhusishana katika fursa za kushiriki katika majukwaa na mikutano inayohusu ununuzi wa umma.

"Tumeamua kushirikiana kwa sababu wote tuko katika Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na kazi tunazofanya zinafanana, hivyo tumeamua kushirikiana na kubadilishana katika kutendaji kazi wetu hiyo ilikuwa ni mwaka 2022 na mwaka jana 2023 bodi yetu ya PPRA ilienda Zanzibar na kufanya kikao.

"Baada ya kikao kile viongozi wetu wa pande zote mbili walitoa maelekezo kwamba tukutane na tuandae makubaliano ambayo yatatuwezesha kushirikiana na kuwezesha pande zote mbili kufanya kazi," alisema.

Maswi alisema wanasheria kutoka pende zote mbili wamefanya kazi kwa kushirikiana na wamewasilisha mapendekezo ambayo wameona yanafaa na PPRA imekubali kwamba yanafaa.

Aliongeza kuwa wamekubaliana kupeana msaada unaohitajika kupitia rasilimali walizonazo, kuwajengea uwezo watendaji wa pande zote mbili na kuwaweka pamoja.



Mkurugenzi Mkuu PPRA, Eliakim Maswi.



Mkurugenzi Mtendaji ZPPDA, Othman Juma Othman.

"Baada ya mkataba huu mimi nikitaka mtu kutoka Zanzibar mwenzangu atamruhusu pia akitaka wa hapa kwetu nitamruhusu maana tunataka kubadilisha uzoefu, kutengeneza ushirikiano maalum katika shughuli za ufuatiliaji, ukaguzi na uchunguzi unaojumuisha uchunguzi wa uzingatiaji wa sheria na thamani ya fedha," alisema Maswi.

"Pia tutashauriana kuhusu nyenzo za kisasa za utendaji wa majukumu ikiwemo vifaa vya kielektroniki na vingine vya kazi ya uchunguzi na ufuatiliaji. Tutakuwa na shughuli za pamoja ambazo tunazifanya ikiwemo kikao cha pamoja cha bodi ya Wakurugenzi, kila upande utakuwa na wajibu wa kuzingatia, kufuata na kutekeleza ratiba hiii," alisema.

"Ni wajibu wa pamoja kuandaa dira na ripoti itolewe ili kubuni mikakati ya kuleta tija katika nch yetu. Tumekubaliana kufanya mafunzo ya muda mfupi ya mara kwa mara kwa watendaji wetu wa mamlaka kwenda kwa kila mamlaka kujifunza yanayohusu shughuli za usimamizi wa mali za umma na uondoaji wa mali," alisema.

Kupitia makubaliano hayo, alisema wanaweza kufanya vikao vya pamoja vya dharura kama kuna changamoto imejitokeza ili kuimarisha Muungano na pia watakuwa wanawasiliana kupeana msaada unaohitajika kwa wakati muafaka kwa ajili ya kupeana mbinu za kutatua changamoto.

Naye Othman alisema: "Tunafanya kazi kwa pamoja kwa maslahi ya Watanzania. Tumetia saini makubaliano haya na yunaishukuru Ofisi ya Mwanasheria Mkuu Zanzibar imetoa maoni yake na leo hii yametuwezesha kufika hapa," alisema.

Makamu Mwenyekiti Bodi ya ZPPDA, Ahmed Makame Haji, alisema makubaliano hayo yameishasainiwa lakini hayatakamilika kama hakutakuwa na utekelezaji wake.

"Kama ambavyo tumekubaliana kuna umuhimu mkubwa wa kuhakikisha makubaliano hayo yanatekelezwa na kujiwekea utaratibu wa kuangalia kama makubaliano hayo yanatekelezwa," alisema.

Alisema kuna umuhimu mkubwa kufanya ufuatiliaji na kuangalia kila mwaka walipofikia katika utekelezaji wa makubalaino hayo na pale ambapo watabaini kasoro watazitatua na kuhakikisha wanafikia hayo makubaliano.

Mwenyekiti wa Bodi ya Wakurugenzi PPRA, Dk. Leonada Mwagike, alisema baada ya kusaini mkataba kilichobaki ni utekelezaji kwa wakati ili kuhakikisha thamani halisi ya fedha inapatikana katika ununuzi wa umma .

Aliwataka kuhakikisha wanafanya tathimini ya utekelezaji wa makubaliano hayo mara kwa mara ili kuhakikisha mkataba huo unatekelezeka.

## RC awaonya vijana mijadala isiyo tija

**Na Elizabeth John,** NJOMBE.

MKUU wa Mkoa wa Njombe, Anthony Mtaka, amewataka vijana kujiepusha na mijadala yenye nia ovu ya kuwagawanya Watanzania na kuhatarisha Muungano.

Mtaka aliyasema hayo wakati wa mkesha wa maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, uliofanyika viwanja wa stendi ya zamani mjini hapa.

"Ni vizuri wakati wote vinywa vya vijana wote wa leo vizungumzie maendeleo, vizungumzie uchumi, vizungumzie kujenga taifa ambalo litathubutu kuwa taifa shindani katika Tanzania ya kesho huko duniani," alisema.

"Tufanye hivyo kama ambavyo Mheshimiwa Rais Samia Suluhu Hassan ameeleza kwenye hotuba kuwakumbusha wanasiasa na Watanzania vinywa vyetu vijenge Muungano wetu, mahubiri yetu tuhubiri maendeleo yetu kama taifa," alisema na kuongeza kuwa vijana wanapaswa kuona mipaka iliyopo nchini kuwa ni fursa.

Mkoa wa Njombe pia umefanya maadhimisho ya miaka 60 ya Muungano kwa kupanda miti katika chanzo cha maji Nyikamtwe kilichoko mjini Njombe.

Akizungumza katika hafla hiyo, Mtaka aliwataka wananchi mkoani Njombe kujiepusha na uchomaji moto, vitendo ambavyo vimetajwa kusababisha hasara na kukatisha tamaa.

"Tumeshuhudia hasara nyingi sana kwenye wilaya ya Njombe kwa sababu ya uchomaji ambao zaidi unasababishwa na visasi, makusudi au bahati mbaya mtu anaenda kusafisha shamba lake mabua anachoma moto unamshinda. Matokeo yake unaunguza maekari ya watu ambao wamewekeza kwa muda mrefu," alisema Mtaka.

Katibu Tawala Mkoa wa Njombe, Judica Omari, alisema mkoa huo ni wa pili kwa upandaji miti na utunzaji wa mazingira.

Ofisa Misitu Wilaya ya Njombe, Audatus Kashamakula, alisema miti 1,000 imepandwa katika chanzo cha maji Nyikamtwe.

# NIDA yatoa vitambulisho kwa Watanzania milioni 20

**Na Enock Charles**

MAMLAKA ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) imesajili zaidi ya watu milioni 24 tangu kuanza kwa mchakato wa usajili wa vitambulisho hivyo mwaka 2012 huku zaidi ya watu milioni 20 wakipatiwa namba ya utambulisho.

Akizungumza na waandishi wa habari jijini Dar es Salaam juzi, Mkuu wa Kitengo cha Mawasiliano wa NIDA, Geoffrey Tengeneza, alisema pamoja na changamoto mbalimbali zilizojitokeza katika mchakato huo, mamlaka imesajili asilimia 79 ya watu wenye umri wa miaka 18 na kuendelea.

Tengeneza alisema NIDA ilibadilishana takwimu na taasisi 96 za umma na binafsi kutoka Tanzania Bara na taasisi tatu kutoka Zanzibar ili kurahisisha upatikanaji wa taarifa za watu binafsi na kuwahudumia wananchi kwa urahisi.

"Hadi kufikia Februari, mwaka huu, NIDA imefanikiwa kusajili watu 24,495,804 ambao ni asilimia 79 ya watu wenye umri wa miaka 18 na kuendelea katika watu 31,477,938 wenye sifa za kusajiliwa.

"Lakini pia tumefanikiwa kutoa namba za utambulisho wa taifa (NIN) kwa watu 20,832,225 ambao ni sawa na asilimia 85 ya watu waliotambuliwa na kusajiliwa. Mamlaka pia imezalisha vitambulisho 20,286,420 ambavyo ni asilimia 97.4 ya watu waliokuwa na namba ya utambulisho," alisema.

Tengeneza alisema mamlaka hiyo imejitahidi kuwapunguzia wananchi tatizo la upatikanaji kadi za NIDA kwa kuzalisha vitambulisho kwa kasi zaidi sasa na kupunguza tatizo la upatikanaji wake jambo ambalo alikiri kuwa ni changamoto ya muda mrefu.

"Sote tulishuhudia jinsi wananchi walivyokuwa wakilalamikia kutopatikana kwa kadi hizo hali inayowakwamisha kupata huduma mbalimbali za kijamii. Tumefanikiwa kukabiliana kabisa na tatizo hili kwa kuhakikisha tunazalisha na kutoa kadi kwa watu wote waliojiandikisha.

"Kama mamlaka tulijipanga kuhakikisha tatizo la uhaba wa kadi za NIDA linapatiwa ufumbuzi kabisa kabla ya kuadhimisha miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar kwa kuweka mikakati miwili ambayo ni utengenezaji wa vitambulisho vya NIDA kwa wingi na usambazaji kwa wingi wa vitambulisho hivyo. ," aliongeza.

Alisema NIDA imewapa wafanyakazi wake utaalamu wa kuunda na kuzalisha kadi ili kuokoa gharama na kuokoa muda unaohitajika kutatua matatizo ya kiufundi yaliyojitokeza wakati wa awamu za uzalishaji walipokuwa wakitegemea wazalishaji kutoka nje ya nchi.

"Uendelezaji wa uwezo wa ndani wa kiufundi ulituwezesha kujikwamua kutegemea makandarasi wa kigeni kuja kutatua matatizo yetu.

Kwa bahati nzuri, sasa tunaweza kufanya kila kitu. Tumewawezesha wataalam wetu kujifunza jinsi ya kuboresha mifumo yetu na kuunda rejista ya kielektroniki yenye taarifa za watu," alisema

# DC awasihi Watanzania kulinda, kuenzi Muungano

**Na Marco Maduhu,** KISHAPU

MKUU wa Wilaya ya Kishapu, Joseph Mkude, amewasihi Watanzania kuendelea kuuenzi na kulinda Muungano kwa vizazi vyote ili kuendelea kufurahia amani, umoja na mshikamano.

Waasisi wa Muungano, Hayati Abeid Amani Karume, ambaye alikuwa Rais wa kwanza Zanzibar na Hayati Julius Nyerere, Rais wa kwanza Tanganyika, waliunganisha Tanganyika na Zanzibar Aprili 26, 1964 na kuwa Tanzania.

Mkude alisema hayo juzi kwenye mkesha wa kusherehekea miaka 60 ya Muungano wilayani hapa.

Alisema Watanzania wanaposherehekea miaka 60 ya Muungano, hawana budi kuwaenzi waasisi hao kwa kuendelea kudumisha amani,mshikamano,upendo na umoja ili nchi iendelee kuwa tulivu na kusongambele kimaendeleo.

Pia alisema kupitia Muungano huo, hali ya ulinzi na usalama inaendelea kuimarika kwa pande zote na amani kuendelea kutawala, huku akiwapongeza marais wote hadi wa sasa, Dk. Samia Suluhu Hassan na Dk. Husein Mwinyi kwa kuendelea kuuenzi na kuulinda Muungano.

Kaulimbiu katika Sherehe za miaka 60 ya Muungano inasema: "Miaka 60 ya Muungano wa Tanzania, Tumeshikamana, Tumeimarika kwa Maendeleo ya Taifa Letu".

# Lissu aibua sakata bei sukari kupanda

**Na Jaliwason Jasson,** BABATI

MAKAMU Mwenyekiti wa Chama cha Demokrasia na Maendeleo (CHADEMA) Taifa, Tundu Lissu, ametishia kutaja hadharani vigogo wanaosababisha bei ya sukari na bidhaa zingine kuwa kubwa.

Amebainisha kwamba vigogo hao wanawabana waagizaji wa bidhaa waongeze cha juu kwa maslahi yao.

Lissu alitoa kauli hiyo jana wakati akihutubia wananchi wa Babati mara baada ya kushiriki maandamano.

"Waagizaji wa sukari wanaambiwa wakiagiza kila kilo moja iwepo Sh. 200 ya kiongozi kutoka Ikulu," alidai na kusema endapo watabisha hilo, kuna siku atawataja wote wanaohusika, hivyo kusababisha bei ya sukari na bidhaa zingine kupanda.

"Bei ya sukari inaongezeka kwa kuwa bidhaa zote zinaongezewa cha juu kwa ajili ya viongozi ndiyo maana tunaumia kwa bei za bidhaa kupanda," alisema.

Pia alisema tozo na unyanyasaji unaofanyika kwa wananchi unaanzia serikalini kwa kuwa hakuna kinachopitishwa na Bunge bila kuanzia huko akitolea mfano tozo za simu.

Kuhusu kikokotoo alisema kitaendelea kuwaumiza wafanyakazi kwa kuwa hawawezi kugoma kwa sababu Shirikisho la Wafanyakazi Tanzania (TUCTA) limerithiwa kutoka iliyokuwa Jumuiya ya Wafanyakazi Tanzania (JUWATA) iliyokuwa chini ya Chama Cha Mapinduzi (CCM).

Lissu alisema iwapo katiba ingekuwa nzuri, wafanyakazi wasingeingia kwenye matatizo ya kikokotoo. Alisema katiba mpya ndiyo itaondoa umungu mtu na kuleta Bunge ambalo litakuwa huru.

Katibu Mkuu wa zamani wa CHADEMA, Dk. Willibroad Slaa, akihutubia mkutano kwa njia ya simu, alisema licha ya kuwa na miaka 60 ya Muungano bado mjamzito akienda kujifungua anaambiwa alipie Sh. 100,000.

Dk. Slaa aliwaomba radhi kwa kutokushiriki maandamano kutokana na shida ya miguu inayomsumbua. Aliwaomba kujiandikisha kwa njia ya kidijitali ili kushiriki uchaguzi wa serikali za mitaa.

Wakili Boniface Mwabukusi aliibua sakata la bandari kwa kusema wapende wasipende bandari iliyouzwa itarudishwa.

Mwabukusi alisema wataandaa maandamano ya kurudisha bandari ambayo itarudishwa kwa nguvu ya umma.




Mratibu wa Idara ya Dharura (ERT) kutoka GGML, Mohamed Mwaimu (wa pili kushoto), akiwaonyesha mamalishe namna ya kuzima moto mtungi wa gesi unapolipuka wakati wa mafunzo yaliyotolewa na kampuni hiyo kwa kushirikiana na OSHA kwa mama lishe 50 wa jijini Arusha mapema wiki hii. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Wataalamu wa kilimo wakutana kuweka mtazamo afya mimea

**Na Ashton Balaigwa,** MOROGORO

WIZARA za Kilimo za Muungano na ile ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar, zimekutana na kubainisha maeneo ya kuoanisha na kuandaa ramani ya kuwa na uboreshaji wa mtazamo mmoja katika usimamizi wa afya ya mimea ndani ya Tanzania.

Mkurugenzi wa Mipango, Sera na Utafiti wa Wizara ya Kilimo, Umwagiliaji, Maliasili na Mifugo Zanzibar , Makame Kitwana Makame, alisema juzi mjini hapa kuwa wakati wa kikao maalumu kilichowakutanisha wadau wa sekta ya kilimo kutoka pande mbili za Muungano.

Wataalamu walioshiriki katika mchakato wa kuoanisha ni wasimamizi wa sera, wapanga mipango, timu za kisheria kutoka Mamlaka ya Afya na Viuatilifu vya Mimea Tanzania (TPHPA) na wawakilishi kutoka Wizara za Kilimo Muungano na na Zanzibar.

Kihistoria, masuala yanayohusu kilimo hayakuwa miongoni mwa masuala ya Muungano, hivyo kuifanya kila sehemu ya Tanzania kuwa na sheria na utekelezaji wake wa kulinda afya ya mimea.

Makame alisema Zanzibar na Tanzania Bara kwenye masuala ya uhifadhi wa mimea wanajaribu kuona ni kwa kiasi gani kunakuwa na taratibu za pamoja zitakazowezesha kufanya biashara nje ya nchi katika mazao ya mimea na miti kwa ujumla.

Alisema Zanzibar iko kweye hatua ya mwisho kuifanyia mapitio sheria ya mwaka 1967 ya Zanzibar inayotoa mwongozo wake na yale ambayo walianza kukubaliana tangu mwaka 2009 kufanyiwa maboresho na sasa yameingizwa katika sheria ya Zanzibar .

Makame alisema Tanzania Bara ilifanya mabadiliko ya sheria yake mwaka 2020 ambayo imetoa miongozo na undani wake inafanana isipokuwa kila upande kitaasisi zimetofautiana.

Mtaalamu Mshauri wa Masuala ya Udhibiti wa Mimea wa Shirika la Chakula na Kilimo la Umoja wa Mataifa (FAO) nchini Tanzania, Dk. Monday Ahonsi alisema ikiwa mlezi wa Mkataba wa Kimataifa wa Kulinda Mimea (IPPC), FAO ina jukumu muhimu katika kuhakikisha uzingatiaji wa viwango vya kimataifa vya hatua za usafi wa mazingira.

Dk Ahonsi alisema IPPC inalenga kudhibiti kuenea kwa wadudu na magonjwa ya mimea kwa njia ya shehena, kuwezesha biashara salama inayozingatia kilimo.

Dk Ahonsi alisema katika kukabiliana na hali hiyo, Mradi wa Kuimarisha Huduma za Afya ya Mimea Tanzania ulianzishwa kwa ufadhili wa Umoja wa Ulaya, FAO na Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania.

Alisema chini ya mradi huo, jumla ya EUR 10,500,000 zimetolewa kwa ajili ya kushughulikia masuala yaliyotolewa katika ukaguzi ili kuimarisha upatikanaji wa mazao ya kilimo salama na bora kwa soko la kitaifa na kimataifa.

Alisema matokeo muhimu yanayotarajiwa ya mradi ni pamoja na kutimiza majukumu ya viwango vya kimataifa, kuboresha uwezo wa wakaguzi wa afya ya mimea, mifumo ya ugunduzi na ufuatiliaji inayofanya kazi.

Alitaja eneo lingine kuwa ni kuimarisha taratibu za uchukuaji sampuli na maambukizi, kuimarisha huduma za ulinzi wa mimea shambani, na kuendeleza mbinu za kisasa za ukusanyaji na uhamishaji data.

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ratiba kombe la Muungano iwe katika kalenda maalum

**MASHINDANO** ya kuwania Kombe la Muungano ambayo hushirikisha timu zilizofanya vizuri kutoka Tanzania Bara na Visiwani Zanzibar yamerejea rasmi mwaka huu.

Mashindano hayo ambayo miaka ya nyuma yalitoa wawakilishi wa Tanzania katika michuano ya kimataifa inayoandaliwa na Shirikisho la Soka Afrika (CAF), yalikuwa hayajafanyika kwa kipindi cha miaka 20.

Kesho ndio mechi ya fainali ya mashindano hayo kwa mwaka huu itachezwa kati ya Simba dhidi ya mshindi kati ya Azam na KMKM. Simba imetinga fainali baada ya kuifunga KVZ ya Zanzibar mabao 2-0. Hata hivyo kutokana na ratiba kuwa finyu, michuano ya mwaka huu imeanzia hatua ya nusu fainali.

Badala ya kufanyika kama ilivyozoeleka miaka ya nyuma ambayo ilishirikisha timu nane, nne kutoka kila upande na mashindano hayo kuonekana kuwa na ushindani, lakini kila timu ilijiandaa vyema kuhakikisha inabeba ubingwa na wakati huo huo inapata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa lakini pia kujenga heshima.

Zanzibar kupata uanachama CAF na timu zake kupata tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika na Kombe la Shirikisho Afrika, ni moja ya sababu zilizopelekea kufutwa au kutofanyika kwa michuano hiyo, lakini pia migogoro kati ya waliokuwa viongozi wa Chama cha Soka Tanzania (FAT sasa TFF) na wenzao wa Zanzibar (ZFA sasa ZFF), pia kulichangia 'kuua' mashindano ya Kombe la Muungano.

Udhamini kutoka katika makampuni yanayozalisha vinywaji vya pombe ambayo hayakuwa yakiruhusiwa kudhamini timu au mashindano huko Zanzibar ni sababu nyingine iliyofanya pia michuano hiyo 'kuzikwa' hapa nchini.

Kama vile imeonekana mashindano ya mwaka huu yamekuwa ya zima moto, inadaiwa mabingwa watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga wamejitoa katika michuano hiyo kwa sababu ambazo hawakutaka kuziweka wazi.

Taarifa zaidi zinadai Yanga imejitoa kwa sababu haitaki kuharibu 'furaha' yake ya kumfunga mtani wake Simba, baada ya kumfunga michezo yote ya Ligi Kuu msimu huu, maana ndani ya siku chache, timu hizo mbili zingeweza kukutana katika fainali ya Kombe la Muungano, hivyo Yanga 'imechomoa' kushiriki na imeweka wazi sasa inaweka nguvu zake katika kuhakikisha inatetea ubingwa wa Bara wanaoushikilia.

Na katika kuonyesha mashindano hayo ya Kombe la Muungano kwa mwaka huu hayakuwa katika ratiba rasmi kwenye msimu wa mwaka 2023/2024, imelazimika Bodi ya Ligi Kuu Tanzania (TPLB), kuahirisha mechi kati ya Simba dhidi ya Dodoma Jiji iliyopaswa kuchezwa Aprili 23, mwaka huu na sasa kupangiwa siku nyingine, ili kuruhusu kikosi cha Wekundu wa Msimbazi kwenda Zanzibar kushiriki michuano hiyo.

Ni ngumu kusema michuano hiyo ya mwaka huu ilikuwa katika kalenda ya mashindano na endapo Simba na Yanga zingefanikiwa kutinga hatua ya nusu fainali ya mashindano ya kimataifa ya Ligi ya Mabingwa Afrika, je michuano hiyo ingekuwepo?

Umefika wakati kwa Kamati ya Mashindano ya TFF na ZFF kukaa pamoja na kupanga kalenda rafiki ambayo itawezesha michuano hiyo kufanyika kila mwaka na kanuni zake zikawekwa hadharani.

Kwa kufanya hivyo, mashindano ya Kombe la Muungano yatarejesha heshima yake na kufanya timu zitakazofuzu kujipanga kuonyesha ubora wake na yasirejee tena kwa kushtukiza kama yalivyofanyika mwaka huu.

Na katika kuhakikisha yanafanyika katika kuendeleza soka na mshikamano wa pande hizi mbili za Tanzania, kwa maana halisi ya kudumisha Muungano, pia yaandaliwe mashindano yatakayohusisha na timu za wanawake, ambayo yanaweza kusaidia wachezaji kupata maandalizi kuelekea michuano ya kimataifa ya Afrika Mashariki na Kati.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
THE GUARDIAN LIMITED
**Mhariri Mtendaji :** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko.** Dennis Ntaita. 0713 578284.
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0677-020701
**Baruapepe:** advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
www.epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge



Na Adam Fungamwango

### Simba isiruhusu kufanya usajili bila Benchikha

**ZIPO** tetesi kuwa klabu ya Simba inataka kuachana na kocha wake mkuu, Abdelhak Benchikha.

Ingawa klabu imekanusha na wengi hawaamini hilo, lakini katika klabu hizi kubwa lolote linawezekana kwa sababu kuna siasa nyingi sana.

Inawezekana tu kwamba wakamtimua ili kuzima joto la wanachama na mashabiki ambao wengi hawaridhishwi, si mwenendo wa klabu tu, bali hata uongozi wa viongozi wenyewe.

Viongozi wa Simba wamekuwa kwenye shinikizo kubwa wakitupiwa lawama kila kona kuwa kwa kiasi kikubwa wao ndiyo wanaosababisha timu kuvurunda.

Nafahamu, moja kati ya mbinu zinazotumiwa na viongozi wa klabu hizi zenye wanachama na mashabiki wengi ni 'kumtoa mtu kafara' ili kupunguza kama si kuzima joto lililopo.

Ukiangalia ndani ya klabu ya Simba huwezi kuona kosa la Benchikha, zaidi kuliko yale ya viongozi.

Baadhi ya viongozi wa Simba wamehusika na usajili karibuni madirisha sita, lakini wamekuwa wakileta wachezaji ambao hawakidhi matakwa, na huwezi kukosea kusema hawana hadhi ya kuichezea klabu kubwa kama hiyo.

Itakuwa ni kichekesho kikubwa, Simba kumuondoa Benchikha, ambaye yeye binafsi ana rekodi nzuri zaidi kuliko klabu yenyewe.

Naweza kuamini pia kuwa huenda baadhi ya viongozi wa Simba wanataka kumtimua ili kupata mwanya wa kusajili wachezaji bila ya kuwa na kocha kama ilivyotokea kwenye msimu kadhaa ya hivi karibuni.

Moja ya sababu kubwa ya Simba kutokuwa na usajili mzuri ni kuchukua wachezaji wakati timu haina kocha.

Sina kumbukumbu nzuri ya nyuma sana, lakini tangu ujio wa Zoran Maki, alikuta wachezaji wamesajiliwa na wengine wanaendelea kusajiliwa.

Hakukaa sana, akaja Roberto Oliveira, ambaye inaonekana kabisa hakushirikishwa kwenye usajili, badala yake alileletewa tu kundi la wachezaji.

Benchikha naye amekuja katikati ya ligi akiwa amekuta wachezaji ambao haihitaji wake kwenda kusomea ukocha kujua kuwa baadhi wametumika sana, wamechanganyikana na wenye umri mkubwa, unajumlisha na wale ambao hawana viwango vya kuchezea timu kama hiyo, hapo utapata timu ambayo inakwenda tu, Mungu nisaidie.

Huwezi kumhukumu Benchikha ambaye amekuja kukuta kuna wachezaji wanaochezea timu hiyo tangu 2013 na wengine 2014 ambao ni tegemeo na ukatarajia akupe matokeo.

Nimesikia Rais wa Heshima na Mwekezaji wa Klabu hiyo, Mohamed Dewji, alikaa na kocha huo kuangalia namna ambayo wanaweza kufanya msimu utakapomaliza, hasa kuhusu usajili wa wachezaji wa msimu ujao. Hilo ndilo linalotakiwa kufanya na si kumtimua kocha aliyekuta wachezaji waliosajiliwa na viongozi.

Inawezekana kabisa baadhi ya viongozi wa Simba wangetamani Benchikha aondoke ili wapate uhuru ule ule wa kusajili wachezaji bila ya kuwa na kocha. Unajiuliza kwa manufaa ya nani? Na kwa nini?

Nafikiri, huenda Benchikha anaweza kuwa yupo Simba kwa sasa kutokana na nguvu ya Mo, na si baadhi ya viongozi.

Huenda kuna wanaonufaika kwa usajili ambao hufanywa bila ya kuwa na kocha. Wanajisajilia tu kiholela. Kila mmoja analeta mchezaji wake.

Nadhani ifike wakati kocha huyu ambaye ni mkubwa Afrika, aachwe ili apendekeze wachezaji anaotaka waachwe na anaopenda wasajiliwe.

Kocha huyu ndiyo anaweza kuitengeneza Simba mpya hata kama huko mbele ya safari ataondoka, ataiacha ikiwa moto kama walivyoifanya Patrick Aussems na Sven Ludwig Vandenbroeck kiasi kwamba makocha wengi waliokuja baada ya hapo walikuwa wanatembelea nyota zao, kwani waliwakuta wachezaji bora na wenye viwango vya juu kutokana na usajili walioufanya.

Atataka wachezaji wa kuja kuipambania timu kutwaa mataji ili alinde wasifu wake na kuipa heshima klabu.

Wachezaji wa aina hiyo mara nyingi huwa wanagharimu pesa nyingi. Gharama yake ni kubwa, nadhani kuna watu pale Simba wanaona kama hilo linaweza kuwakosesha ulaji.

Wanachofanya sasa ni kutengeneza propaganda ili kosa aonekane hafai aondoke, wawe huru.

Kwa bahati nzuri propaganda hiyo imegonga mwamba. Kulikuwa na mpango wa kutaka kumchafua kocha ili aonekane hafai. Walitaka kufanya kile kinachoitwa, 'ikitaka kumuua mbwa, mpe jina baya.'

Bahati nzuri, wanachama na mashabiki wa Simba hakukubali kitu hiki. Chawi wao wanamjua.

Nina uhakika, Benchikha akikaa na kupendekeza usajili wake, msimu ujao Simba itarejea kuwa ya kutisha na kuheshimika.

HABARI PICHANI

# SHEREHE ZA MIAKA 60 YA MUUNGANO WA TANGANYIKA NA ZANZIBAR KATIKA PICHA



Rais na Amiri Jeshi Mkuu wa Majeshi ya Ulinzi na Usalama, Samia Suluhu Hassan akikagua gwaride la heshima lililoandaliwa na Jeshi la Ulinzi la Wananchi wa Tanzania (JWTZ), wakati wa Sherehe za Miaka 60 ya Muungano wa Tanganyika na Zanzibar, katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam jana. **PICHA: IKULU**



Waziri wa Maendeleo ya Jamii, Jinsia, Wazee na Watoto Zanzibar, Riziki Pembe Juma akimpokea Rais wa Namibia, Dk. Nangolo Mbumba alipowasili katika Uwanja wa Ndege wa Kimataifa wa Julius Nyerere, kwa ajili ya kushiriki sherehe za miaka 60 ya Muungano, jana. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**



Sehemu ya viongozi mbalimbali pamoja na wananchi waliohudhuria sherehe hizo. **PICHA: IKULU**



Rais Samia Suluhu Hassan akihutubia wananchi na viongozi mbalimbali, wakati wa sherehe hizo. **PICHA: IKULU**



Sehemu ya viongozi mbalimbali pamoja na wananchi waliohudhuria sherehe hizo. **PICHA: IKULU**

# Waziri ataka kuimarishwa klabu za kidijitali shuleni

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Waziri wa Wizara ya Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari Mhandisi Maryprisca Mahundi amewahimiza wakuu wa shule za awali, msingi, sekondari na vyuo vikuu kuanzisha klabu za kidijiti shuleni.

Pia amesema klabu hizo zitahamasisha vijana kuwa na ujuzi wa teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) utakaosaidia kutafuta suluhu za kiteknolojia za changamoto mbalimbali kwenye jamii zinazotuzunguka pamoja na kutumia TEHAMA kukuza uchumi wa kidigiti na kujikwamua kiuchumi.

Mahundi alisema hayo jana wakati wa Maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wasichana na TEHAMA yaliyofanyika mkoani Arusha.

Alisema serikali itaendelea kuunga mkono jitihada zilizopo katika kuongeza idadi ya wasichana wanaochukua masomo ya sayansi na kuwaandaa ili waweze kunufaika vizuri na Uchumi wa kidigiti.

Akizungumza kwenye maadhimisho hayo yaliyoongozwa na Kaulimbiu ya "Uongozi", Naibu Waziri Mahundi aliipongeza Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kuratibu maadhimisho hayo yenye lengo la kuhamasisha uongozi katika TEHAMA hususani kwa wasichana ili kusogeza ulinganifu wa kijinsia.

Awali, Mwenyekiti wa Bodi ya TCRA, Dk. Jones Killimbe, alisema anatambua mchango wa wadau mbalimbali katika kuwezesha upatikanaji wa huduma za mawasiliano na kukuza maendeleo ya sekta ya mawasiliano.

Aliongeza kuwa ukuaji wa teknolojia unategemea na kuwepo kwa mazingira wezeshi kwa wasichana ili kuendeleza bunifu zao.

Mkurugenzi Mkuu wa TCRA, Dk. Jabiri Bakari, alisema ni muhimu wasichana kujikita katika utengenezaji wa mifumo na programu za kiteknolojia, kusoma masomo ya uhandisi, kujikita katika tafiti za teknolojia mpya kama Akili Mnemba (Artificial Intelligence- AI) na kuwa sehemu ya wataalamu wa masomo ya TEHAMA wa ngazi zote za elimu na baadaye kushiriki kwenye kutunga sera hasa katika eneo hilo la TEHAMA.

Alisema takwimu zinaonyesha kukua kwa kasi kwa sekta ya mawasiliano nchini ambapo hadi kufikia Machi, 2024 kumekuwa na laini za simu milioni 75 kutoka laini za simu milioni 61 mwezi Juni mwaka 2023 ambalo ni sawa na ongezeko la asilimia 13.

Dk. Jabiri alisema takwimu za Machi pia zinaonyesha kuongezeka kwa watumiaji wa intaneti kwa asilimia 8.3 kutoka watumiaji milioni 34 mwezi Juni mwaka 2023 hadi kufikia milioni 36.8 mwezi Machi mwaka 2024.

Alitaja baadhi ya sababu zinazochangia ongezeko hilo kuwa ni matumizi ya intaneti ambayo pia yamechangia kuwa na maudhui mengi ya Kiswahili, uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu umefanyika kwenye teknolojia zote yaani 2g, 3g, 4g na 5g.

Aidha, alisema teknolojia ya huduma za intaneti kwa kutumia nyaya yaani fiber imechangia kuongezeka kwa matumizi ya intaneti ambapo takribani watumiaji elfu 49 wananufaika na teknolojia hiyo majumbani (Fiber To Home) huku watumiaji zaidi ya elfu 5 wakinufaika na teknolojia hiyo maofisini (Fiber To Office).

Alisema takwimu za utangazaji zinaonyesha kumekuwa na ongezeko la ving'amuzi na ongezeko la watoaji huduma za maudhui mtandaoni huku huduma za Posta na usafirishaji wa vipeto zikiwa zimeongezeka na hivyo kuchagiza ukuaji wa biashara mtandao yaani e-commerce.

Kuhusu ubora wa huduma za mawasiliano Dk. Jabiri alisisitiza ni kutokana na jitihada zilizofanywa na serikali kwa kushirikiana na watoa huduma katika kuboresha huduma za posta, utangazaji, simu na intaneti kwa kuwa ni muhimu katika kuleta maendeleo ya taifana kuchangia kuimarika kwa miundombinu ya kidigiti na kuchangia kwenye ukuaji wa kiuchumi.

Aliongeza kuwa TCRA itaendelea kutoa taarifa za mwenendo wa ukuaji wa sekta ya mawasiliano kila baada ya miezi mitatu, ili wadau waweze kuwa na uelewa wa pamoja wa ukuaji wa sekta hiyo.



Mwenyekiti wa Umoja wa Wazazi wa CCM Mkoa wa Morogoro, Dk. Rose Rwakatare (wa pili kulia), akipata maelezo ya ujenzi wa ofisi za CCM Wilaya ya Kilombero, kutoka kwa Katibu wa chama hicho Wilaya, Joseph Mwambeleko, alipotembelea wilayani humo, juzi. Wa (tatu kulia) ni Mwenyekiti wa CCM Wilaya hiyo, Mohamed Msuya. PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE

# PASADA yakumbuka waathirika mafuriko

Na Joyce Lameck

SHIRIKA lisilo la kiserikali linalojihusisha na utoaji wa huduma kwa watu wanaoishi na virusi vya UKIMWI (PASADA), limetoa msaada wa vifaa vyenye thamani ya Sh. milioni nane kuwasaidia waathirika wa mafuriko katika wilaya za Rufiji na Kibiti.

Shirika hilo lililo chini ya Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, lilitoa msaada huo juzi jijini Dar es Salaam ambao baadaye ulipelekwa kwenye maeneo hayo kwa ajili ya kugawa kwa waathirika.

Misada iliyotolewa na PASADA ni pamoja na magodoro na ndoo zenye koki kwa ajili ya kuwasaidia waathirika hao kuishi katika mazingira safi ili kujiepusha na magonjwa yatokanayo na mafuriko.

Akizungumnza wakati wa ibada maalumu ya kuviombea vifaa hivyo, Askofu Msaidizi Kanisa Katoliki Jimbo Kuu la Dar es Salaam, Henry Mchamungu, alitoa wito kwa mashirika mengine nchini kujitokeza kuunga mkono juhudi za kuwasaidia waathirika.

Askofu Mchamungu alilishukuru shirika hilo kwa kuguswa na kutoa mchango wa vitu ambavyo vitawasaidia kutokana na athari zilizowakumba wakazi wa maeneo hayo.

"Ninawashukuru PASADA kwa moyo wao wa kujitoleo magodoro pamoja na ndoo zenye koki ambazo zitasaidia katika usafi, kama tunavyojua kuwa mafuriko huwa yanaambatana na magojwa ya mlipuko.

"Pamoja na PASADA kutoa msaada huo, Jimbo Kuu la Dar es Salaam bado linajipanga kwa ajili ya kutoa msaada kwa wale walioathirika na mafuriko katika maeneo hayo," alisema Mchamungu

Mkurungezi wa Huduma na Tiba wa PASADA, Eugene Filbert, alisema lengo la kutoa vifaa hivyo ni kuzisaidia familia zilizokumbwa na mafuriko.

Pia alitoa wito kwa viongozi wa maeneo hayo kuhakisha vifaa hivyo vinawafikia walengwa walioathiriwa ili kuwasaidia katika kipindi hiki kigumu wanachopitia.

Mkurungezi Mtendaji wa Pasada, Cayus Mrina, alisema lengo la kutoa msaada huo ni kuunga mkono juhudi za serikali katika kupambana na maafa.

# Watumishi wafundwa mbinu kabla kustaafu

Na Mwandishi Wetu

NAIBU Katibu Mkuu Wizara ya Fedha, Jenifa Omolo, amewataka watumishi wa umma kutimiza majukumu yao kwa wakati na weledi na kuwekeza kwa ajili ya maisha ya uzeeni ili kuepuka usumbufu katika kipindi cha kustaafu.

Omolo alitoa wito huo juzi wakati wa Mkutano wa 37 wa Baraza la Wafanyakazi Wizara ya Fedha mwaka 2023/24, kwa niaba ya Katibu Mkuu wa Wizara hiyo, Dk. Natu Mwamba, katika ukumbi wa Kilimanjaro, Benki Kuu ya Tanzania (BoT), jijini Dar Es Salaam.

"Ni vyema ukamaliza majukumu yako kwa wakati husika ili angalau miezi miwili kabla ya kustaafu kila kitu chako kiwe sawa. Si mpaka siku chache kuelekea kustaafu bado una majukumu mengi hujayakamilisha", alisema.

Omolo alisisitiza kuwa ni vyema watumishi wakawekeza wakati wakiwa kazini ili kuhakikisha kuwa wanakuwa na uwezo wa kuendesha maisha na kukidhi mahitaji yao muhimu baada ya kustaafu.

"Mada ya uwekezaji ni muhimu sana kama ilivyowasilishwa wafikishieni watumishi wote umuhimu wa kuwekeza, tunaweza kuwekeza UTT AMIS, bima na benki lengo ni kuhakikisha kuwa tunavyofanya kazi tuwe na namna ya kuwekeza kwa ajili ya familia zetu na kujiandaa kustaafu", alisisitiza.

Naibu Katibu Mkuu aliongeza kuwa kuwa uongozi wa wizara hiyo utahakikisha unatatua changamoto mbalimbali zinazoweza kukwamisha utendaji wa watumishi na kuhakikisha wanapata stahiki.

Pia aliwataka watumishi hao kushiriki kikamilifu katika kutekeleza bajeti iliyopitishwa kwa kufanya kazi kwa bidii ili kuunga mkono juhudi zinazofanywa na Serikali za kuleta maendeleo ya nchi.

Mkutano wa Baraza la Wafanyakazi wa Wizara ya Fedha hufanyika kila mwaka ambapo hutoa fursa kwa watumishi kujadili na kuwasilisha changamoto mbali mbali katika maeneo ya kazi ili ziweze kutatuliwa.



# Wajipanga kuleta mapinduzi ya kilimo

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

WADAU wa kilimo ikolojia hai wamejipanga kuleta mageuzi kwenye sekta ya kilimo nchini kwa kutengeneza mpango kazi wa mwaka 2024/25 kwa ajili ya utekelezaji vipaumbele vya mkakati wa kitaifa wa kilimo hai wa ikolojia wa 2023-2030 (NEOAS).

Akizungumza juzi kwenye kikao hicho kilichoratibiwa na Mwavuli wa Taasisi za Kilimo Hai Tanzania (TOAM), Mkurugenzi wa Sera na Mipango wa Wizara ya Kilimo, Obadia Nyagiro, alisema kilimo hicho ni muhimu kwa watanzania kwa kuwa kitaleta tija kiuchumi, kulinda afya za walaji, afya ya udongo na kuongeza kipato.

Alisema mkakati huo unatokana na Sera ya Kilimo kuelekeza masuala ya kuweka mfumo wa uzalishaji, upatikanaji wa masoko na kutambua bidhaa za kilimo hai.

Nyagiro alisisitiza kuwa serikali itaendelea kutoa ushirikiano ili kufanikisha uandaaji wa mpango huo kwa kuwa ni muhimu wadau kushiriki katika kilimo himilivu na endelevu kwa mazingira na afya ili kuleta tija kwenye sekta ya kilimo.

Alizitaka asasi za kiraia na sekta binafsi kuchangamkia fursa ya uwekezaji katika kilimo hicho kwa kuwa kina tija kubwa.

"Nihimize sekta binafsi na asasi za kiraia mpitie na kuona fursa ya kuwekeza katika eneo hili kwa kuwa tija yake ni kubwa ikiwamo kuongezeka kwa mapato, mkipitia nchi nyingine mtaona waliowekeza kwenye kilimo hiki na tija yake na ni muhimu mipango yetu izingatie kilimo himilivu kinachozingatia mabadiliko ya tabianchi," alisema.

Naye Mwenyekiti wa TOAM, Dk. Mwatima Juma, alisema kilimo hicho kinalenga kuwa na uzalishaji wa kutosheleza kulinda afya na udongo kwa kuondokana na matumizi ya kemikali.

"Kilimo cha kutumia kemikali kilianza miaka 100 iliyopita baada ya kuisha kwa Vita Kuu vya Pili vya Dunia ambapo utengenezaji wa mbolea za kemikali, viuatilifu vya kemikali ilionekana itatusaidia kuzalisha chakula zaidi.

"Tulihamasika kuwa kutumika kemikali ndo ukisasa na kwa bahati mbaya tuliacha kilimo chetu cha asili ambacho mtu alikuwa akilima kahawa ndani yake ana kunde,maharage, mtama vyote vinazalishika vizuri na ana ng'ombe anatupia mbolea shambani kwake," alisema.

Aliongezak uwa: "Tukahamasisha tuwe na mashamba makubwa tulime zao moja, tupulize dawa miaka imekwenda na tulipofika mimi binafsi nasema tuwaombe radhi wakulima kwa maeneo tuliyowapeleka hasa wakulima wadogo hapafai, kuna aina ya ukulima wanaweza kulima bila kupunguza uzalishaji, bila kupata shida kwenye chakula na kuuza kwenye masoko ya ndani na nje.

Alibainisha kuwa kilimo hicho kitasaidia watanzania kuondokana na maradhi mbalimbali ikiwamo uzazi, saratani kwa kuwa yanatokana na matumizi ya kemikali kwenye kilimo.

Naye Paul Holmbeck kutoka Shirika la Biovision Foundation akizungumzia mataifa mengine namna yanavyotekeleza kilimo hicho, alisema wanasayansi na mashirika ya kimataifa ya masuala ya kilimo yanahimiza kilimo hicho kwa usalama wa chakula na kuna tija kiuchumi ambapo serikali za nchi ambazo zinatekeleza kilimo hicho zinaweka malengo yake.

# Madereva wadai kutozwa faini bila risiti

**Na Thobias Mwanakatwe,** SINGIDA

MADEREVA na wamiliki wa bajaji na pikipiki za abiria, maarufu kama bodaboda, katika Manispaa ya Singida wamelalamikia kutozwa faini ya Sh. 30,000 katika kipindi cha miaka miwili kwa ajili ya maegesho na mfanyabiashara aliyepewa zabuni na halmashauri bila risiti za malipo.

Madereva na wamiliki hao waliwasilisha kilio hicho juzi kwa Mkuu wa Mkoa wa Singida, Halima Dendego, ambaye alikuwa akizungumza nao katika viwanja vya Bombadia kwa ajili ya kusikiliza kero zinazowakabili na kuzitafutia ufumbuzi.

Katibu wa Chama cha Madereva na Wamiliki wa Pikipiki Manispaa ya Singida (CHAMWAPITA), Abiud Mlowezi, alisema: "Kero kubwa kwetu ni kuandikiwa faini ya maegesho ya Sh. 30,000 wakati hapa manispaa hakuna 'parking'."

Naye Mwenyekiti wa CHAMWAPITA, Abdi Mitigo, alisema tatizo la kutozwa faini hizo za maegesho lilianza tangu 2022 na kitendo cha kutopewa risiti kinatia shaka huenda fedha hizo zinaingia kwenye mifuko ya watu.

Kutokana na hali hiyo, Dendego, alipiga marufuku madereva hao kulipa tozo yoyote bila kupewa risiti kwa kuwa ni kinyume cha utaratibu wa serikali.

Alisema ni jambo la aibu kwa watendaji wanaokusanya mapato ya serikali na kutotoa risiti wakati msisitizo mkubwa wa serikali ni kuwa malipo ya aina yoyote lazima mnunuzi apewe risiti halali ili serikali ipate mapato kwa ajili ya kutekeleza miradi ya maendeleo. "Haiwezekani kwa serikali tuwe wa kwanza kutotoa risiti hilo halipo na haitawezekana tunataka haki bin haki. Mkurugenzi wa Manispaa ya Singida ukakae na mzabuni ili muweke utaribu wa kutoa risiti kama Serikali inavyoelekeza," alisema.

Dendego pia alimwagiza mkurugenzi wa manispaa kukaa na viongozi wa madereva hao kuwasaidia kuanzisha Chama cha Kuweka na Kukopa (SACCOS) ili kukopa fedha kwa ajili ya kununua vyombo vyao vya usafiri badala ya kuendesha vya watu hali ambayo itawasaidia kuboresha maisha yao.

Alisema kwa sasa chama chao ambacho kina zaidi ya wanachama 4,000 kinaweza kukopeshwa na kurejesha mikopo kwa haraka kama watendaji watawasaidia kuanzisha SACCOS yao.




Naibu Waziri wa Viwanda na Biashara, Exaud Kigahe (kushoto), akiangalia mbegu bora ya alizeti kwenye banda la wakulima na wazalishaji katika kongamano na tamasha la kitaifa la alizeti Tanzania, jijini Dodoma juzi. Kulia ni Mkurugenzi wa kiwanda cha Naki Group, Annamaria Leone. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# Mkakati wazinduliwa kuongeza tija wakulima uzalishaji shayiri

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

MPANGO mkakati wa kusaidia wakulima wa shayiri Tanzania umezinduliwa ili kuongeza uzalishaji wa zao hilo na kukidhi soko la viwanda vya ndani na biashara katika ukanda wa ndani.

Akizungumza baada ya kuzinduliwa kwa mkakati huo, Mkurugenzi Msaidizi kutoka Idara ya Maendeleo ya Mazao Wizara ya Kilimo, Beatrice Banzi, alisema mkakati huo unaweka kipaumbele maeneo matano.

Alisema maeneo hayo ni upatikanaji wa mbegu, kuwahamsisha na kuwaunganisha wakulima kupitia ushirika na mifumo mingine na kuboresha masuala ya miundombinu ikiwamo masoko ya shayiri.

"Eneo lingine la mpango huu ni kuboresha sera na sheria katika masuala ya uzalishaji na biashara ya zao la shayiri na masuala ya kilimo cha mkataba. Kwa sasa kumekuwa kama mwiba kwa wakulima, mnunuzi na mzalishaji, hivyo kupitia mkakati huu tutatibu hili tatizo la kwa nini mikataba yetu inakuwa haina tija kati ya mkulima, mnunuzi na mzalishaji. Kwa mantiki hiyo, utekelezaji wa mpango mkakati huu utafuatwa hatua kwa hatua utaongeza uzalishaji wa shayiri," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Nafaka na Mazao Mchanganyiko (COPRA), Irene Mlola, alisema mkakati huo umelenga kuhakikisha Kampuni ya Bia ya TBL inanunua zao hilo kwa wakulima wazawa na shayiri inayozalihwa ikidhi mahitaji kwenye ubora na kiwango kinachohitajika.

"Wadau wa maendeleo Shirika la Fedha la Kimataifa (IFC) na mnunuzi mkubwa ambaye ni TBL. Hawa wadau wote wanaohusika na mnyororo wa thamani kwa zao la shairi tumekuja na mkakati huu," alisema.

Naye Mwakilishi wa IFC, Sam Nganga, alisema taasisi yake itaendelea kusaidia mpango huo ili kuwasaidia wakulima kuondokana na tatizo la upatikanaji wa fedha, uzalishaji mdogo wa mazao na kuzalisha kwa ubora.

Mkurugenzi Mtendaji wa TBL, Michelle Kilpin, alisema hatua hiyo itawezesha kuongeza uzalishaji wa tani 3,500 za shayiri hadi kufikia tani 20,000 kwa wakulima.





# Mwinyi ahimiza jitihada kutokomeza malaria

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

RAIS wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi, amesema ni muhimu wananchi kuzingatia maelekezo ya wataalamu wa afya juu ya kujikinga na malaria ili kufikia lengo la kumaliza maradhi hayo nchini ifikapo mwaka 2029 kama unavyoelekeza Mpango Mkakati wa Kumaliza Malaria wa miaka sita (2024-2029).

Amesema licha ya kwamba kwa sasa malaria inaendelea kupungua, bado kuna baadhi ya maeneo hususan katika wilaya za Mjini, Magharibi 'A' na 'B' Unguja, inaendelea kuisumbua jamii.

Dk. Mwinyi aliyasema hayo juzi kwenye maadhimisho ya Siku ya Malaria Duniani, akiwakilishwa na Waziri wa Afya, Nassor Ahmed Mazrui.

"Hali hii haikubaliki na hatua madhubuti zichukuliwe kudhibiti maambukizi ya malaria kwa kushirikisha sekta zote nchini," alisema Dk. Mwinyi.

Alisema serikali itaendelea kuhakikisha upatikanaji wa huduma zote muhimu za afya zinazohitajika kudhibiti malaria zinatolewa kwa wananchi.

Dk, Mwinyi alitoa wito kwa mikoa yote ambayo bado ina maambukizi ya malaria kuhakikisha inasimamia vizuri utekelezaji wa mikakati sahihi ya kumaliza malaria katika maeneo yao ili hatimaye Zanzibar ifikie lengo kuu la kutokomeza maradhi hayo.

Alisema hilo linawezekana kwa kuhakikisha usimamizi mzuri wa utekelezaji wa afua za kupambana na malaria zinatekelezwa kikamilifu na kwa ufanisi.

"Nawahimiza wananchi kulala ndani ya vyandarua vilivyotiwa dawa na kuendelea kuwahi kufika katika vituo vya afya ili kupatiwa huduma mapema pindi tu wanapojiskia na dalili za maradhi haya. Na wanapokutwa na maambukizi ya malaria kuhakikisha wanakamilish dozi kamili ya ugonjwa wa malaria," alisema.

Pia alisema bado kuna haja kubwa pia ya kuelimisha jamii juu ya usafi wa mazingira ili kupunguza mazalia ya mbu na kujikinga na malaria.

"Natoa wito kwa idara na taasisi zinazosimamia sheria ya afya ya jamii na mazingira na kanuni zake kuhakikisha wanasimamia vizuri utekelezaji wa sheria na kanuni hizo," alisema.

Dk.Mwinyi pia alizindua kampeni ya ugawaji vyandarua kwa nchi nzima na katika mpango huo, shehia 314 za Unguja na Pemba zitanufaika.

Vyandarua 782,000 vimenunuliwa kupitia Mfuko wa Rais wa Marekani wa Kupambana na Malaria (PMI) na viliaanza kugawiwa kwa jamii.

Mkurugenzi Mkazi wa Shirika la Misaada ya Maendeleo la Marekani (USAID), Craig Hart, alisema PMI) itaendelea kushirikiana na Tanzania kupambana na kumaliza malaria.

Alisema ufadhili huo umewasilisha vyandarua vyenye viatilifu, dawa za kuokoa maisha, upimaji wa kiwango cha juu na kutoa mafunzo kwa wafanyakazi wa afya.

Alisema kupitia ushirikiano wa karibu na watu, taasisi na serikali ya Tanzania, serikali ya Marekani pia imeimarisha mifumo ya afya kuimarisha na kuongeza juhudi za kumaliza ugonjwa huo hatari, lakini, unaoweza kuzuilika.

Wakati huo huo, Dk. Mwinyi alizindua Baraza la Kumaliza Malaria Zanzibar ambalo lengo kuu ni kuhakikisha nchi inakuwa na uwezo wake wa kuwa na vyanzo vya mapato ya ndani ili kusaidia juhudi ya kumaliza malaria.




Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Udhibiti wa Ununuzi wa Umma (PPRA), Eliakim Maswi (kulia) na Mkurugenzi wa Mamlaka ya Ununuzi na Uondoaji wa Mali za Umma Zanzibar (ZPPDA), Othman Juma Othmani wakitiliana saini makubaliano ya kufanya kazi kwa pamoja, jijini Dodoma jana. **PICHA: JOSEPH MWENDAPOLE**

# Waziri aitwisha zigo ALAT maslahi ya umma

**Na Rahma Suleiman,**
ZANZIBAR

WAZIRI wa Nchi Ofisi ya Rais Tawala za Mikoa,Serikali za Mitaa na Idara Maalum za SMZ, Masoud Ali Mohammed, ameziitaka Jumuiya za Tawala za Mikoa (ALAT) kujipambanua kwa kutetea maslahi ya umma ili kuleta mabadiliko ya kweli kwenye jamii.

Waziri Masoud alisema hayo juzi wiki wakati akifunga Mkutano wa Mkuu 38 wa ALAT, uliofanyika visiwani hapa.

Alisema kama viongozi wa jumuiya hawatakuwa wakweli na kuendelea kuoneana aibu, ni ndoto kuleta mabadiliko yanayotarajiwa na wananchi.

"ALAT ni chombo muhimu ambacho kinatakiwa kusimamia uadilifu, kupambana na ubadhirifu wa mali za umma, kutetea maslahi hasa ya wanyonge," alisema Waziri Masoud.

Aliwataka wajumbe wa ALAT kujitahidi kujenga serikali za mitaa zenye uwajibikaji, uwazi na zenye kusikiliza sauti za wananchi kwa kusimamia rasilimali zilizopo.

Waziri Masoud alisema changamoto nyingi zinazotokea kwa wananchi, ALAT ndiyo wa kwanza wanaotakiwa kuzitafutia ufumbuzi kabla ya kufika serikali kuu.

Pia Waziri Masoud aliishukuru ALAT kwa namna ilivyofanya jitihada kubwa katika kuanzishwa kwa Jumuiya ya Tawala za Mikoa Zanzibar (ZALGA).

Alisema ushirikiano baina ya ZALGA na ALAT ni muhimu katika kuhakikisha kwamba sauti za mamlaka za serikali za mitaa zinapaishwa katika kuwaletea maendeleo wananchi.

"Niwasihi ushirikiano huu uendelee kudumishwa ili kuhakikisha tunafikia malengo ya sera hii" alisema Waziri huyo.

Mwenyekiti wa ALAT, Murshid Ngeze, alisema ni vyema mikutano ya ALAT ifanyike kabla ya vikao vya Bunge na Baraza la Wawakilishi ili hoja zitakazoibuliwa ziweze kujadiliwa katika vikao hivyo.

"Hii itasaidia kwa wajumbe waliopo katika vikao hivyo kutoa mawazo yao na kuchukuliwa ili kufanyiwa kazi katika kipindi cha bajeti bungeni".alisema.

## Wakutana kufanikisha Mbio za mwenge Zanzibar

**Na Mwandishi Wetu**

WAJUMBE wa kamati za Mbio za Mwenge wa Uhuru wa mikoa ya Unguja, wamekutana kujadili maandalizi ya mbio hizo ambao unatarajiwa kuwasili Mei 17, mwaka huu, ukitokea Mkoa wa Kaskazini Pemba.

Akizungumza jana baada ya ufunguzi wa kikao hicho makao makuu ya polisi mkoa wa Kusini Unguja, Tunguu, Mwenyekiti wa Kamati hiyo, ambae pia ni Mkuu wa Mkoa Kusini Unguja, Ayoub Muhammed Mahmoud, aliwataka viongozi na watendaji kuendeleza ushirikiano wa pamoja katika harakati zote za maandalizi ili shughuli za mbio hizo zinafanikiwa.

Alisema mafanikio ya Mbio za Mwenge wa Uhuru ni chachu katika kukuza maendeleo ya jamii na taifa kwa jumla pamoja kutoa ujumbe kwa jamii kuhusiana na kuendeleza mabambano kujikinga na maradhi yakiwamo UKIMWI na malaria pamoja na athari za mazingira na utumiaji wa dawa ya kulevya kwa vijana.

"Kwenye mbio hizo za mwenge wa uhuru miradi mbalimbali ya maendeleo itazinduliwa na mengine kuwekewa mawe ya msingi lakini pia huambatana na ujumbe kwa jamii katika mapambano ya maradhi mbalimbali jinsi ya kujikinga na kuchkua tahadhari," alisema Ayoub.

Wajumbe hao waliahidi kuzidisha ushirikiano ili shuguli hiyo ya kitaifa kufanikiwa na kupata maendeleo.

Wajumbe hao, akiwamo Rashid Hadid Rashid, Mkuu wa Mkoa wa Kaskazini Unguja, walisihauri kurejeshwa kwa utaratibu wa awali wa kuwekwa vikao vya tathmini kuanzia ngazi za mikoa hadi taifa baada ya kumalizika kwa mbio hizo ili kubaini changamoto na kufanyiwa kazi kwa wakati.

Ujumbe wa mwaka huu wa mbio za mwenge wa uhuru ni 'Tunza Mazingira na Shiriki Uchaguzi wa Serikali za Mitaa kwa Ujenzi wa Taifa Endelevu'.



**MSIKIENI JOSELYN ANACHOSEMA** UKURASA 14



Nipashe
MWANGA WA JAMII
BT
BURUDANI TELE



# JAY MELODY Huyu hapa....

MWANAMUZIKI mwenye sifa ya kuimba kipekee Jay Melody, anatarajia kutambulisha Albam yake mpya inayoitwa 'Therapy' na kumfanya kuwa msanii wa kwanza kuimba kwa nyimbo zake zote lugha ya Kiswahili.

Wakati mashabiki wake wamesubiri kwa hamu muda ufike, Jay Melody, amesema yuko tayari kuwapatia wapenzi wake tiba ya muziki ambayo itawaacha wakiwa na furaha muda wote.

Baadhi ya wadau wa muziki wamemuelezea msanii huyo kama mtu mwenye sifa na misimamo mikali kwa kutokubali kubadili aina ya muziki wake.

Adam Shauri ambaye ni mtaalamu wa muziki, amesema Jay Melody ana sifa za kipekee kutokana kubaki katika muziki wa Bongo Fleva asilia na imekuwa vigumu kushawishika na aina nyingine ya muziki kama Amapiano.

Amesema kiualisia Jay Melody, hana tabia ya kutaka kuchanganya muziki wake na ndio maana hana kolabo nyingi na wanamuziki wengine.

Hata hivyo amemshauri msanii huyo kupunguza msimimamo mikali na kukubali kuwashirikisha wanamuziki wengine katika kazi zake kwani kwa sasa licha ya kuwa na jina kubwa, lakini anapiga hatua polepole.

BASI SAWA

## Rhino kwa Mungu habanduki



MSANII wa bongo fleva, ambaye kwa sasa amegeukia muziki wa Injili, Rhino King, amesema anafurahia maisha ya kumuimbia Mungu kuliko muziki wa kidunia.

Amesema kutokana na kuwa na furaha kwa sasa, hakumbuki chochote kama alikuwa akipanda kwenye majukwaa na kuimba nyimbo za kidunia.

"Yale yaliyopita kwangu hayana nafasi tena kwa kuyazungumzia, kuyafikiria wala kuyaishi, huku nina familia bora sana inayonizunguka," amesema msanii huyo.

## Atim wambea wanasubiri ubuyu



MKE wa zamani wa mwanamuziki wa Uganda, Jose Chameleone, Daniella Atim, amekuwa kwenye shinikizo kali kutoka kwa mashabiki wake wakimtaka kuelezea namna maisha yao ya ndoa yalivyokuwa kabla ya kutalakiana.

Atim amezindua chaneli yake katika mtandao wa YouTube ambayo itaendasha kipindi chake cha masuala ya ndoa na anatarajia kuzungumzia mambo mbalimbali mazuri na mabaya yaliyotokea wakati wa uchumba na kuolewa na Chameleone,

Hata hivyo, kilichowashangaza wengi ni hatua ya kuita kipindi chake kwenye chaneli hiyo kuwa 'Diary of a retired wife' kwa maana kwamba atakuwa anazungumzia maisha kama mke aliyestaafu kutoka kwenye ndoa na staa huyo wa muziki.



## ALBAM YA ZUCHU HIYOO...

MWANAMUZIKI maarufu wa Bongo Fleva, Zuchu, anatarajia kuachia wakati wowote Albamu yake ya kwanza katika safari yake ya kimuziki.

Zuchu ambaye anamilikiwa na lebo ya WCB, amepata umaarufu ndani ya miaka minne katika maisha yake ya muziki, lakini hakutoa Albam kama walivyofanya wanamuziki wengine walioinukia kwa muda wa hivi karibuni.

Akizungumzia ujio huo, mwanamuziki huyo amesema kwamba ndani ya Albam hiyo kutakuwa na nyimbo mbalimbali ambazo amewashirikisha wasanii wa ndani na nje ya nchi.



## Phina aonyesha tititi

JANA saa nne asubuhi, msanii mwimbaji wa kike anayefanya vizuri kwa sasa Phina, ametambulisha ngoma yake aliyoipa jina la 'Tititi.'

Video ya ngoma hiyo mpya iliachiwa katika majukwaa ya muziki kwa ajili ya kukidhi nyoyo za mashabiki wake ambao walikuwa wanasubiri kwa hamu.

"Nilikufuata huku nalia, kufuata wako msamaha baby, ila wewe ukanichunia, sijui ulitaka mimi 'nidedi', ulitingisha kibiriti, mimi bado nipo fiti." Ni baadhi ya maneno yaliyomo katika ngoma hiyo ambayo maudhui yake ni ya mgongano au mgogoro wa mapenzi baina ya wapenzi wawili.

FILAMU

# Diana: Tezi na omo marejeo ngamani



**Na Adam Fungamwango**

MTUNZI wa filamu ya 'Diana', aliamua kutengeneza kitu hiki ili kutoa elimu kwa jamii kuwa penzi siku zote haligawanyiki, lakini pia utazunguka kote, lakini utarudi ulikotoka. Waswahili wa Pwani wanasema, mwenda tezi na omo, marejeo ngamani.

Imechezwa na wasanii mbalimbali mastaa kama Single Mtambalike "Richie', Sabrina Rupia 'Cathy', Halina Yahaya 'Davina' na wengineo.

Inaanza kuonyesha Richie akiishi kwa amani na upendo na familia yake, akiwa na mke na watoto wake wawili.

Hata hivyo, anaanza kuingiwa na shetani, kumpenda sekretari wake Davina.

Richie ambaye ni bosi kwenye kampuni, anatumia cheo chake kumnasa mrembo huyo.

Davina anakuwa 'nyumba ndogo', lakini siku zote penzi halina siri, baadhi ya wafanyakazi wanaanza wakaelewa mchezo mzima na siri ikapenyezwa kwa mkewe.

Mke wa Richie, anavamia ofisini na kupelekwa kinyemela sehemu ambayo wapenzi hao wanapata chakula cha mchana.

Mke anatembeza mkong'oto kwa mwizi wake na kumchania nguo, huku akimchimba mkwara mzito wa kutishiwa maisha.

Kitendo hicho kinamuumiza mno Davina, anaamua kuua uhusiano, Richie alitumia rupia kurudisha penzi.

Mapenzi yao kila yalivyozidi kushamiri, ndivyo walivyozidi kuiumiza familia. Mke wa watoto wa Richie hali ikawa mbaya kwani walikosa chakula na ada ya shule.

Siku zote muonja asali huchonga mzinga, Davina alichoshwa na tabia ya kutukanwa mara kwa mara na mke wa bosi wake, hivyo akataka aue ndege wawili kwa jiwe moja. Amkomoe Cathy, lakini pia ammiliki moja kwa moja Richie.

Akaenda kwa mganga kumroga mke wa bosi wake na kweli, Cathy akapata ugonjwa wa kupooza.

Kunatokea upotevu wa pesa za kampuni na kusababisha Richie afukuzwe kazi. Ugonjwa wa mkewe, kuyumba kiuchumi kikasababisha atake kujiua.

Hata hivyo rafiki yake anamshauri asifanye hivyo, badala yake akampeleka kwa mganga ili kuangalia kama kuna mikosi iondolewe.

Huko anakutana na mpenzi wake Davina ambaye anakimbia alipomuoa.

Mganga anamwambia msichana aliyekimbia alikuwa akija kuchukua dawa ya kuroga kwani anatembea na mume wa mtu.

Richie anamwambia kuwa mtu anayerogwa ni yeye na familia yake, kitu ambacho kinamshangaza mganga.

Baada ya mazungumzo ya muda mfupi wanagundua kuwa wanafahamiana na walishawahi kusoma shule moja miaka ya nyuma.

Mganga anampa Richie dawa ya kumponyesha mkewe na kumuondolea mikosi ili arejeshwe kazini.

Anarejea nyumbani kwake na alipofika hapo, ghafla mkewe alirejea na nguvu, akasimama. Furaha ikarejea ndani ya familia kwani mke amepona. Richie akarejesha upendo kwenye familia na kuachana na Davina.

# WANAPIGANA TEMBO, ZINAUMIA NYASI

**Na Adam Fungamwango**

NDOA kuvunjika kwa sasa si ajabu sana hata barani Afrika, tofauti ya miaka ya nyuma ambako tuliliona sana hili kwenye mabara ya wenzetu, hasa Ulaya.

Hata hivyo, katika bara hili ambako wazazi wanakuwa na watoto wengi, wao ndiyo waoathirika zaidi.

Wanaume pia wana tabia ya kutelekeza familia na kuacha jukumu hilo kwa mke, huku akizuzuliwa na 'nyumba ndogo', lani pia kuna baadhi ya kinamama wenye tabia kama hiyo.

Hapa tunawaletea nyimbo ambazo wanamuziki waliangalia matatizo ya aina hiyo.

Wanawake walielezea jinsi walivyoachwa na waume zao wa watoto, wakibaki na kazi ya kulea watoto

Wanaume nao walielezea jinsi wanavyopata shida kulea watoto baada ya kuachana au kukimbiwa na wake zao.

### Ule Baba Watoto-Lovy Longomba

Mwanamuziki Lovy Longomba, katikati ya miaka ya 1980, aliimba wimbo uitwao 'Ule Baba Watoto.'

Ni kwamba Ule alimuacha mkewe na watoto wanateseka, akahama nyumbani akawa anaishi kwenye nyumba za starehe, akiiacha familia yake inateseka. Hapo sasa mkewe analalamika juu ya kuachwa na mumewe, akimuachia jukumu la kuilea familia. Huyu baba yanaweza kumkuta mbele ya safari akalalamika.

### Mama Watoto-Les Wanyika

Kwenye wimbo huu ni kwamba mwanamke ameondoka nyumbani na kumwachia mwanaume watoto.

Mume anapelekea ujumbe, kama wa barua au wa simu sijui. Lakini anamwambia kuwa arejee nyumbani ili alee watoto. Kwenda kazini, halafu akiwa na jukumu la kulea watoto yeye kwake limekuwa gumu. Mama huyu naye anaweza baadaye kudhani watoto wake hawampendi.

### Mama Feli-Cosmas Chidumule

Ni mwanaume anayemtoa wasiwasi mkewe kuwa tetesi anazozisikia kama anataka kuoa mke mwingine si kwa ukweli. Anamwambia mkewe kuwa hawezi kufanya hivyo kwa sababu familia itasambaratika na malezi ya watoto yatakuwa si mazuri.

Mara zote furaha ya watoto ni kuona baba na mama wapo pamoja, lakini hali inapokuwa tofauti, watoto nao wasambaratika na kulelewa upande mmoja.

Hii inasababu hata watoto wenyewe kuegemea upande mmoja ule ambao amelelewa na kusahau upande mwingine wa mzazi.

### Mundinde-Hemed Maneti

Kwenye wimbo huu, Maneti akiwa na Vijana Jazz anakwenda kumpasha jirani yake mmoja juu ya vitendo vya kwenda kumwambia maneno maneno mkewe.

Anamwambia hata kama amemuona na wanawake wengine, haipaswi kwenda kumwambia mkewe kwa sababu anaweza kuvunja ndoa.


Anamwambia kidudu mtu huyo Mundinde kwamba wakiachana watakaotesema si wao, ni watoto ambao watalelewa vibaya na baadaye kutokuwa na misimamo kwenye maisha yao.

### Kupatwa kwa mwezi-Mwenge Jazz

Ni wimbo ambao baba anamuelezea mtoto wake ni kwa nini mama yake hayupo nyumbani hapo.

Anamwambia ukweli kuwa mama yake ametoroka na amempata mwanaume mwenye pesa nyingi na ameondoka nyumbani pale kwa makeke na matusi mengi dhidi yake na kumuacha hata yeye akiwa bado mdogo.

Anampoza mtoto wake kuwa usiwe na wasiwasi, kwani ataishi vizuri na atampata mama mwingine hivi karibuni.





# Msikieni Joselyn anachosema..

MSANII wa filamu na mtangazaji wa televisheni, Joselyn Dumas, amesema akina mama wasio na waume wanapata changamoto nyingi wakati wakijaribu kupata wapenzi wapya.

Wakati wa mazungumzo yake, Joselyn alisimulia tukio lake kibinafsi lililohusisha rafiki yake wa kiume ambaye alionyesha kusitasita kuchumbiana na mwanamke mwenye mtoto akihofia kuchukua majukumu ya malezi ya mtoto ambaye si wake kibaiolojia.

Amesema changamnoto hizo zinachangia akina mama wengi wasio na waume kubaki waseja.



## Abraham ananyanyua vyuma

MWIGIZAJI maarufu kutoka nchini Ghana, Abraham Attah, ameibua mjadala baada ya picha aliyoiweka kwenye Instagram kuonekana yuko tofauti na siku za nyuma.

Picha hiyo ambayo inamonyesha akitoka kuoga, alionekana mwili wake umejaa misuli ya mazoezi na kusababisha mashabiki wake kutoa maoni tofauti kuhusu mwonekano wake mpya.

Msanii huyo ambaye alijipatia umaarufu katika filamu ya Beast of Nation, ameonekana kuwa na furaha kuwa na muonekano huo na kuandika kwamba sasa amekuwa mtu mzima na anatakiwa kubadilika.

## Baba Ijesha akata rufani

MAHAKAMA ya Rufaa nchini Nigeria, imepokea rufani iliyokatwa na mwigizaji wa Nollywood ,Baba Ijesha, kufuatia hukumu ya kifungo cha miaka 16 jela aliyopewa na Mahakama Kuu ya Jimbo la Lagos.

Baba Ijesha ambaye alipatikana na hatia ya unyanyasaji wa kingono dhidi ya mtoto, aliiomba mahakama ya rufaa kutengua hukumu hiyo kwa kuwa anaona hakuwa na hatia.

Jopo la watu watatu wa mahakama ya rufaa, likiongozwa na Jaji Folasade Ojo, lilisikiliza rufaa yake na kisha kuahirishwa kusikilizwa hadi tarehe nyingine itakayopangwa.





## Zulu amemaliza mwendo

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Zulu Adigwe amefariki dunia juzi.

Msanii huyo ambaye alipata umaarufu kwa nafasi yake katika filamu ya Ken Saro-Wiwa, inayoitwa Basi and Company (1987), alifariki siku ya Jumanne, lakini haijaelezwa sababu ya kifo chake.


Habari hizo zilithibitishwa na mtayarishaji wa filamu Stanley Nwoko, ambaye kwenye Instagram yake aliandika "Najuta kutangaza kuaga kwa mwigizaji mkongwe, marehemu Zulu Adigwe. Chanzo cha kifo chake bado hakijafahamika,"

## Kanye kwa hili unazingua

RAPA maarufu nchini Marekani, Kanye West, amewashangaza mashabiki zake baada ya kutangaza kuingia rasmi katika kuandaa video za ngono.

Kupitia ukurasa wake wa X (zamani Twitter) aliweka video fupi yenye ujumbe kuwa Aprili 4, anaingia katika tasnia hiyo ya Ponografi.

Siku chache zilizopita mtandao wa TMZ uliripoti msanii huyo anapanga kuzindua studio ya ponografi, ambao utakuwa sehemu kwa ajili ya watu wazima.





## HABARI KASKAZINI

# Tanzania yapaa kwa huduma mawasiliano

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

TANZANIA imekuwa na maendeleo makubwa ya huduma za mawasiliano kwa gharama nafuu, kwa mijini na vijijini kwa kufanikisha kutoa laini za simu milioni 72.5 hadi kufikia Machi mwaka huu.

Vilevile, katika kipindi hicho idadi ya watumiaji wa mitandao ya Intaneti imekua hadi kufikia watu milioni 36.8

Hayo aliyasema jana jijini Arusha Naibu Waziri wa Habari, Mawasiliano na Teknolojia ya Habari, Mhandisi Maryprisca Mahundi, alipokuwa kwenye maadhimisho ya Siku ya Kimataifa ya Wasichana na Tekniolojia ya Habari na Mawasiliano (TEHAMA).

"Idadi kubwa ya watanzania wa mijini na vijijini imefikiwa na huduma ya mawasiliano ya simu na mitandao ya Internet, haya ni maendeleo makubwa katika sekta ya mawasiliano hapa nchini,"alisema.

Alisema idadi hiyo ni kubwa kufikiwa katika utoaji wa huduma hizo, ukilinganisha na nchi zingine.

Pia alisema upatikanaji wa huduma hizo kumewezesha jamii ya watanzania kushirikia ipasavyo uchumi wa kidijiti.

"Mazingira haya ya upatikanani wa huduma hizi yanawezesha upatikanaji wa huduma za kijamii kwa urahisi na kusaidia kuzalisha ajira na kufungua fursa mbalimbali mpya kwenye kilimo na maeneo mengine, kwa ajili ya maendeleo endelevu ya kiuchumi," alisema

Pia aliagiza vyuo vikuu,ya kati,shule za sekondari na Msingi kuanzisha klabu za kidijiti ili kuhamasisha wanafunzi kupenda masomo ya Sayansi nabkukuza ujuzi wa kidijiti.

Mkurugenzi Mkuu wa Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania 9TRCA), Dk. Jabir Bakari, alisema lengo la maadhimisho hayo ni kuhamasisha wasichana kuchukua masomo ya sayansi, uhandisi, teknlojia na hisabati na kuwawezesha na kuwaandaa kuja kunufaika na fursa zilizopo,yakiongozwa na kaulimbiu isemayo 'Uongozi.'

"Maendeleo ya dunia ya sasa yameshikiliwa sana na matumizi ya teknolojia katika kila nyanja hivyo ni muhimu wasichana kujikita katika utengenezaji wa mifumo na programu za kiteknolojia, kusoma masomo ya uhandisi,kujikita katika tafiti mpya kama vile akili bandia na kuwa sehemu ya utaalam wa masomo ya Tehama kwa ngazi za elimu na pia kuja kushiriki katika ngazi ya kutunga sera,hasa katika eneo hili la TEHAMA," alisema.

Sekta ya mawasiliano ya simu nchini, alisema imeendelea kukua kwa kasi ambapo hadi Machi mwaka huu laini za simu zilikuwepo milioni 72.5 toka laini laini milioni 64.1 Juni, 2023 sawa na ongezeko la asilimia 13.

Alisema takwimu hizo za Machi zimeonyesha ongezeko la watumiaji wa intaneti kwa asilimia 8.2 toka watumiaji milioni 34 juni mwaka jana hadi kufikia watumiaji milioni 36.8.

"Sababu zilizochangia ongezeko hilo ni matumizi ya intaneti,ambayo yamechangia kuwa na maudhui mengi ya kiswahili,uwekezaji mkubwa kwenye miundombinu iliyofanyika kwenye maeneo mbalimbali,simujanja zimeongezeka kutoka milioni 16.7 Juni 2023, hadi milioni 20.1,Machi mwaka huu ikiwa ni ongezeko la asilimia 20,"alisema.

# TAKUKURU yabaini mianya ya rushwa zabuni ujenzi jiji

**Na Cynthia Mwilolezi,** ARUSHA

MKUU wa Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Mkoa wa Arusha, Zawadi Ngailo, amesema wamebaini uwapo wa mianya ya rushwa kuanzia mchakato wa zabuni ya ujenzi wa jengo la utawala la Halmashauri ya Jiji la Arusha, iliyotangazwa kwa njia ya vikwazo, badala ya zabuni ya wazi.

Jengo hilo la utawala la Halmashauri ya Jiji la Arusha, linatarajia kujengwa kwa gharama ya Sh. bilioni 12.

Akizungumza jana na waandishi wa habari jijini hapa, Ngailo alisema upungufu wa ujenzi wa jengo hilo, ulibainika kwenye uwepo wa mianya ya rushwa kuanzia mchakato wake uliotangazwa kwa njia ya vikwazo.

Alisema baada ya kubaini mapungufu hayo walichukua hatua ya kusimamisha mchakato huo na kulitaka Jiji kutangaza upya kwa njia ya wazi.

Taasisi yake, alisema ilipata taarifa za tukio hilo mwishoni mwa mwaka jana, na kuanza kulichunguza kwa karibu hadi kubaini mapungufu hayo.

"Baada ya kupokea taarifa, tulifanya ufuatiliaji wa zabuni hiyo ambapo pia tulibaini uwepo wa mianya ya rushwa katika mchakato wa uteuzi wa njia ya manunuzi kama inavyoelekezwa na kanuni, na kwenye uundwaji na utekelezaji wa jukumu la uchambuzi yakinifu" alisema.

Nagilo alisema katika ufuatiliaji wa fedha za umma zilizotolewa na serikali kwa ajili ya utekelezaji wa miradi mbalimbali kwa miezi mitatu kuanzia Januari hadi Machi, mwaka huu, pia wamebaini upungufu katika miradi mingine minne. Alitaja upungufu waliobaini kuwa ni kwenye mfumo wa maji katika vyoo vya Shule ya Sekondari ya Lake Eyasi iliyoko Karatu, unaojengwa kwa thamani ya Sh. milioni 584 na ujenzi wa Shule ya Sekondari Kamwaga iliyoko Longido wenye thamani ya zaidi ya Sh. milioni 580.

"Katika miradi hii miwili, tuliagiza kamati ya ujenzi wa shule hizo, zisimamie urekebishwaji wa miundo mbinu hiyo kwa kuzingatia kiwango cha ubora," alisema. Pia alitaja upungufu mwingine katika ujenzi wa mtaro wa barabara ya Mtaa wa Naurei, Kata ya Sekei Wilaya ya Arumeru, wenye thamani ya Sh. milioni 30 na ujenzi wa nyumba za walimu sita katika Shule ya Maweni iliyoko ndani la Jiji la Arusha, unaotekelezwa kwa Sh. milioni 70.

"Tumeelekeza miradi hii yenye upungufu yote ifanyiwe marekebisho na maboresho.,lakini pia kwenye ujenzi wa mtaro wa Naurei, kwanza mradi umecheleweshwa na hakuna vibao vya tahadhari. Kwa ujenzi wa nyumba moja ya walimu sita kuna dosari katika malipo ya zaidi ya Sh. milioni 2.4 yaliyofanywa na mzabuni na vyote tumebaini upungufu na wahusika wamekubali na wanarekebisha," alisema.



Mkuu wa Mkoa wa Manyara, Queen Sendiga (aliyechuchumaa), akizungumza na wazee wa kijiji cha Endagaw, wilayani Hanang' juzi, baada ya kutembelea mradi wa skimu ya umwagiliaji. **PICHA: GIFT THADEY**

# Wakili abainisha ukubwa wa tatizo la afya ya akili

**Na Godfrey Mushi, MOSHI**

WAKILI mkongwe nchini na mwanaharakati wa haki za binadamu, Elizabeth Minde, amesema matatizo ya afya ya akili na kiwewe (trauma) hivi sasa yanawaachia maumivu makali Watanzania, huku baadhi yao wakifikia mahali pa kushindwa kufanya kazi, hivyo kuathiri shughuli za uzalishaji.

Akieleza kwa kina juu ya matatizo hayo, alisema matokeo ya afya ya akili na kiwewe, pia kwa sasa yanaathiri na watoa huduma wanaoshughulika kila siku kupokea wateja mbalimbali kwenye masuala ya kisheria.

Minde, ambaye pia ni Mkurugenzi wa shirika lisilo la kiserikali la KWIECO, alikuwa akizungumza jana na wafanyakazi wa shirika hilo, watoa huduma wengine wanaofanya kazi na jamii ya kufanana nao, yakiwamo mashirika ya TUSONGE CDO, NAFGEM na watumishi wa serikali za mitaa ngazi ya kata.

"Impact (athari) ya hivi vitu ni nini jamani, hata kwetu inatuathiri. Kwa hiyo lazima tujue 'management' ya hiyo 'prosses' inakuwaje (namna ya kuhimili huo mlolongo), kwa sababu si tu tunazungumza trauma ya mteja, tunazungumzia trauma ya watoa huduma pia.

"Unapozungumzia afya ya akili, wanakusimulia kama vile wewe ni kichaa, lakini ni kitu ambacho kinatokana na mwingiliano wa matatizo, inakuathiri wewe na inamuathiri na yule aliyekuja kwako, naye ameathirika vilevile," alisema.

Akizungumzia mafunzo ya siku tatu yaliyotolewa ili kujenga uwezo wa pamoja, Mratibu wa Mradi wa Afya ya Akili na Trauma wa Shirika la KWIECO, Immaculate Mworia alisema: "Walionufaika na mafunzo haya ni wafanyakazi wa Shirika la KWIECO, ambao kwa namna moja au nyingine kutokana na majukumu yao ya kila siku wanakuwa wanapokea wateja mbalimbali kwenye masuala ya kisheria.

"Lakini pia ndani yake tukagundua kwamba kuna masuala ya kisaikolojia, ambayo tunakumbana nayo, wakati tunafanya kazi zetu za kuwasaidia wateja wetu kwenye masuala ya kisheria.

"Kwa hiyo tuliona ni vizuri wafanyakazi wakapata haya mafunzo ya namna ya kuhudumia watu wanaokabiliwa na matatizo ya kisaikolojia wakati wakishughulikia masuala ya kisheria; kwa kuweza kuwatambua na pia kufanya rufaa kwenda Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, pale wanapoona kuna masuala ambayo hawataweza kuyashughulikia kutokana na eneo wanalofanyia kazi."

KWIECO iliendesha mafunzo hayo kwa ushirikiano na Shirika la CrossRoad Intenational la Canada.

Kwa mujibu wa Mworia, wadau hao wamefundishwa namna ya kufanya utambuzi wa mtu mwenye matatizo hayo na namna ya kuwasaidia kwa njia ya mazungumzo.

"Wamefundishwa kuhusu self care, watu wanapokuwa kazini jinsi ya kujitunza nafsi, kwa sababu wanakuwa wanafanya kazi YA kuhudumia watu, halafu wanajisahau wao wenyewe,"alieleza zaidi Mratibu huyo.

Daktari bingwa wa afya na magonjwa ya akili wa Hospitali ya Rufani ya Kanda ya KCMC, Dk. Editruda Gamassa, alisema hivi sasa wanapokea wagonjwa wa nje wenye matatizo ya afya ya akili, zaidi ya 300 kwa mwezi mmoja.

Kwa mujibu wa Dk. Gamassa, magonjwa ya afya ya akili, ambayo ni tishio nchini ni Kihoro (Anxiety), Sonona (Depression), PTSD-Trauma (Post Traumatic Stress Disorder), Baipola (BPD), Skizofrenia na Uraibu.

TULIKOTOKA, TULIPO & TUNAKOKWENDA

# Wanavyofunguka, yaliyoko mazikoni..

-Ubishoo, kutambiana, dili za mlo
-Kuonyeshana ustaa, magari ya bei...
-Umbea na vita ndiyo mahala pake
-Anaingizwa kaburini, simu zao bize
-Kulala msibani 'no', wao gesti, baa...

**Na Adam Fungamwango**



MAKALA iliyopita kwenye safu hii iliyokuwa na kichwa cha habari, 'misiba ya sasa, ukilinganisha na zama zile, imebadilika kupitiliza, ' imeonekana kuibua wasomaji wengi sana wa gazeti hili, ambao walipiga simu na kutuma meseji zao walionekama kuguswa mno.

Baadhi walikuwa wanapongeza, lakini wapo walioongezea baadhi ya matukio ambayo wameyashuhudia wao kwenye misiba mbalimbali, inayounga mkono makala ya wiki iliyopita.

Kutokana na wingi wa wasomaji kuonekana kuguswa nimeona leo tena niirudie, lakini kwa kiasi kikubwa nitaweka kile ambacho wasomaji wenyewe wamekileta.

Kabla ya kufanya hivyo, tuweke mambo sawa ili anayesoma kwa mara ya kwanza ajue mada ilikuwa ni nini?

Kiufupi niliandika kuwa mienendo ya watu siku hizi misibani imebadilika kabisa, siyo kama ilivyokuwa zamani.

Niliandika kuwa zamani majirani wanapofika msibani kitu cha kwanza ni kumfariji mfiwa, kuchukua watoto wake wote wenye umri mdogo na kuwaondoa eneo la tukio, wakipelekwa nyumba jirani ambako watafanyiwa kila kitu, wataoga, na watachangishana pesa kuhakikisha waliofika awali kwenye msiba watakula bila wafiwa kutoa hata senti moja, lakini pia walikuwa na walinzi wa wafiwa ili wasiibiwe.

Kikubwa zaidi ni kwamba muda wote watakuwa na mfiwa, wakihakikisha halii moja kwa moja, badala yake kumbembeleza kula chakula, na mahitaji mengine muhimu ili aendelee kuwa na nguvu.

Sehemu yenyewe ya msiba kila mmoja alikuwa na uso wa huzuni na simanzi kiasi kwamba mtu unapopita huwezi hata kuuliza kama kuna msiba au la, pia watu wanaswali, wanasali na kuimba kwa hisia kali.

Kinyume chake, mienendo ya watu misibani siku hizi inahuzunisha kuliko hata msiba wenyewe.

Watu kama wapo kwenye sherehe. Kwenye msiba wa matajiri, watu maarufu au mastaa ni kuonyesha nguo na magari ya gharama.

Mtu anashuka kwenye gari na kwenda sehemu yenye msiba huku anatabasamu, anatembea kwa mbwembwe kama vile anaenda kuweka pesa benki.

Watu wanaendelea na maisha ya kawaida, wanaongea mpira, wanataniana, wanabishana, wengine wanachati na simu mwanzo, mwisho, hakuna tofauti na mtu anavyoshinda sebuleni kwake, kama vile hakuna chochote kilichotokea. Simu ziko bize kupiga picha na kuziposti kwenye akaunti zao.

Kipengele cha kulala msibani, ndiyo kimebadilika balaa. Huwezi amini, kwa sababu hizo hizo, kundi kubwa linajaa gesti za jirani, huku wengine usiku kucha kama hawako 'pub', basi kwenye mechi za Arsenal, na haishangazi simulizi za ndoa nyingi huanzia kwenye matukio hayo.

Huko uani, kinamama wanashindana nani kaja na dela la gharama, na simu ya bei mbaya, ndugu yangu kama umekuja na kitochi, utakoma, utasimangwa na kutetwa mpaka basi.

Kwa sababu nilishaandika sana wiki iliyopita, nawapa nafasi wasomaji ambao walinipigia simu na wengine kutuma meseji zao.

"Hongera kwa kuandika habari za misiba. Kweli tupu, lakini umesahau, utawakuta kinamama wako bize kupika, lakini wakati wa kupakua kabla ya wafiwa hawajapewa chakula, wameshajipakulia chakula chao cha kutosha, nyama kibao, yaani kwao 'full' sherehe, ukichanganya na umbea juu.

Zile pilikapilika za kinamama msibani zifuatilie mimi nimeona misiba zaidi ya 10, shughuli ni hiyo hiyo nakwambia," aliandika msomaji mwenye simu namba 0763 246060.

"Da! Ama kweli, umefafanua tofauti ya zamani na sasa kuhusu misiba, yaani mimi nimeishia kucheka tu, hasa ulipoanza kufafanua kinachofanyika katika misiba ya sasa.

Nini kifanyike kurudisha heshima na staha ya misiba jamani?" Akaandika msomaji anayetumia namba 0717 282109.

"Hujakosea ndugu, vioja vyote msibani wachotaka watu ni kuzika tu basi," aliyeandika hivyo ni msomaji mwenye namba 0757 358484.

"Misiba ya siku hizi watu wanaenda ili mradi tu waonekane na wao walikuwepo, na wala siyo kuomboleza. Ndio maana siku hizi yale matanga ya kulala siku saba hamna tena, mnazika mnaanua tanga kila mtu anatawanyika," alisema msomaji mmoja aliyepiga simu.

"Akina mama ndiyo wanatumia huo muda kuoneshana madera ya gharama, magari, dhahabu na simu. Ole wako usiwe na 'smart phone', utachambwa balaa," mama mmoja alichangia kwa kupiga simu.

"Sasa kuna wale wanaoiga uzungu, kafiwa na mtu wake wa karibu kabisa lakini anathubutu kujiremba, wengine hadi saluni wanaenda! Wengine wavaa nguo, viatu vya bei mbaya na miwani myeusi juu, ubishoo umewajaa, hawalii machozi na kugaragara, wanaona poda au 'enjoy face', itatoka," alisema mwingine.

"Yaani marehemu anaingizwa kaburini, watu simu zao ziko bize, badala ya kuzima, kila mmoja anakwenda kupokea pembeni, tena badala ya kusema wapo msibani, kila mmoja anazungumza bila kujali." Msomaji mmoja alibainisha.

"Siku hizi utakuta msibani baadhi ya wanawake hata kanga havai, eti anavaa suruali, kichwa wazi jamani! Sijui kwa nini?" Ni simu za baadhi ya wasomaji wetu.

"Maigizo yamechukua nafasi bila kusahau wanja na lipstick, kuonyeshana mitindo ya nywele na nguo, huku hisia kiduchu. Hisia zilikuwa zamani jama."

Yupo aliyepiga simu na kuongea kwa hisia sana. "Mkuu, misiba ya sasa imekua majanga sana, yaani badala ya watu kwenda msibani kusitiri na kuwafariji wafiwa badala yake misiba imegeuka vijiwe vya majungu na kuwajadili wafiwa.

Sasa mimi najiuliza kuna manufaa gani kuwajadili wafiwa tena? Zamani misibani watu walikua na heshima sana tofauti na sasa, sijui tunakwama wapi?

Mkuu niombe tuweni mabalozi wa kuikemea tabia hii tuwapo misibani kwa sababu haipendezi kabisa."

Mtu wa mwisho aliyefunga kazi alinipigia simu na kuongea maneno ambayo nayawasilisha hapa.

"Kuna siku ilitokea misiba miwili kijijini kwetu na wote walizikwa siku moja. Kaya moja ilikuwa masikini na nyingine wana kiuwezo uwezo.

Yaani watu walienda kuzika kule kwa masikini chapuchapu, wakaondoka hata bila kumaliza taratibu za kimila, wakawahi kule ambako kulikuwa na vyakula vya kutosha na pombe.

Chakusikitisha waliisimanga sana ile familia masikini, jambo hili liliniuma sana. Misiba imegeuka kuwa sehemu ya maonyesho, na watu wanakuja kula na kunywa. Yaani ukifiwa kama huna milioni kama tano hivi kazi unayo.

Utachekwa mpaka ukome. Yaani wanacheka mpaka aina ya jeneza.

**Tuma meseji 0716 350534**

HABARI KIMATAIFA

# Watu wanne wauawa Rafah

**GAZA,** PALESTINA

MASHAMBULIZI ya anga yaliyofanywa na jeshi la Israel jana kwenye mji wa Rafah katika Ukanda wa Gaza, yamesababisha vifo vya watu watano.

Kulingana na maofisa wa afya wa Palestina, wamesema mashambuzi hayo yamelenga mji huo ulioko kusini mwa Gaza na kuongeza hali ya hofu kwa watu milioni 2.3 waliokimbilia mji huo kwa ajili ya hifadhi.

Jeshi la Israel limekuwa likifanya mashambulizi ya anga karibu kila siku, huku likionekana kujiandaa kwa operesheni kamili ya ardhini katika eneo hilo.

Kulingana na taarifa zilieleza tayari Israel imeweka magari mengi ya kivita na zana mbalimbali za kijeshi karibu na mji huo.

Mbali na vifo hivyo vilivyotokea Rafah, watu wengine wanne wameuawa kutokana na mashambulizi yaliyolenga katikati mwa Ukanda wa Gaza.

Wizara ya Afya inayodhibitiwa na Hamas ilisema tangu kuanza kwa mzozo huo, zaidi ya watu 34,000 wameshauawa, wengi wao wakiwa wanawake na watoto.

Wakati huo huo, ofisa mmoja mwandamizi wa Hamas aliliambia shirika la habari la The Associated Press kwamba kundi hilo liko tayari kufikia makubaliano ya usitishwaji mapigano kwa muda wa miaka mitano au zaidi na Israel.

Hata hivyo, ofisa mwingine wa Hamas alisema kundi hilo litaweka chini silaha ikiwa kutatekelezwa suluhisho la mataifa mawili.

Wakati huo huo, Naibu mkuu wa Shirika la Mpango wa Chakula Duniani (WFP), Carl Skau, amesema eneo la kaskazini mwa Gaza linaelekea kukabiliwa na baa la njaa kwa sababu Israel haijaruhusu kazi ya usambazaji wa chakula kwa mamia ya maelfu ya watu wanaokabiliwa na ukosefu wa chakula.

Skau alisisitiza kuwa tangu Israel iahidi kuharakisha utoaji wa misaada, kuna maendeleo kidogo yaliyopatikana kwa sababu kiwango kinachoruhusiwa hakitoshi kukidhi mahitaji ya watu wa Gaza.

Katika tukio lingine, kundi la Hezbollah limemuua raia mmoja baada ya kufanya mashambulizi ya kuvizia kwa msafara wa jeshi la Israel katika eneo la mpakani linalogombaniwa kati ya nchi hiyo na Lebanon.

Pia, meli iliyokuwa ikisafiri kupitia bahari ya Ghuba ya Aden ilishambuliwa na waasi wa Kihouthi wa nchini Yemen kama kulipiza kisasi kutokana na mashambulizi ya Israel katika Ukanda wa Gaza.

**Dw**



Wapalestina wakiokota vifaa vyao baada ya jengo kuharibiwa na shambulizi la jeshi la Israel jana katika mji wa Rafah.
**PICHA: ALLIA**

## BBC, VOA marufuku Burkina Faso

**OUAGADOUGOU,** BURKINA FASO

SERIKALI ya kijeshi nchini Burkina Faso, imesimamisha kwa muda wa wiki mbili matangazo ya BBC Afrique na Voice of America (VOA), baada ya vyombo hivyo kuripoti mauaji ya wanavijiji yaliyohusishwa na wanajeshi wa nchi hiyo.

Taarifa hiyo iliyoudhi serikali hiyo ya kijeshi ni ripoti ya shirika la kutetea haki za binadamu la Human Rights Watch inayoshutumu jeshi la Burkina Faso kwa kutekeleza dhuluma dhidi ya raia.

Upatikanaji wa tovuti na majukwaa ya kidijitali ya BBC, VOA, na Human Rights Watch pia umesitishwa.

Kulingana na shirika la habari linalomilikiwa na serikali BBC na VOA, kupitia waandishi wao walioko nchini humo wameamriwa kutangaza tena kipindi hicho kwenye majukwaa yao yote.

Baraza Kuu la Mawasiliano (CSC) lilionya vyombo vyote vya habari vya ndani kuacha kusambaza makala hiyo, likitishia kuvifungia kwa kukiuka agizo hilo.

Hata hivyo, VOA ilisema katika taarifa yake kwamba inasimamia utangazaji nchini Burkina Faso na inakusudia kuendelea kufuatilia kikamilifu na kwa haki shughuli zao nchini humo.

HRW ilichapisha ripoti hiyo siku ya Alhamisi ikilishutumu jeshi la Burkina Faso kwa kuwaua raia 223 kaskazini mwa nchi hiyio.

Mnamo Desemba 2023, taifa hilo la Afrika Magharibi lilifungia gazeti la Ufaransa la Le Monde likilishutumu kwa kuripoti kwa upendeleo.

# China yaionya Marekani kwa kuvuka mipaka yake

**BEIJING,** CHINA

WAZIRI wa Mambo ya Nje wa China, Wang Yi, ameionya Marekani dhidi ya tabia yake ya kuvuka mipaka katika masuala mbalimbali na kuvuruga uhusiano wa nchi hizo mbili.

Akizungumza na waziri mwenzake wa Marekani, Antony Blinken, alisema wakati umefika kwa nchi hizo zinatakiwa kufuata mwelekeo sahihi wa kusonga mbele.

Waziri Wang alifungua mkutano huo kwa swali ambalo lilitafsiriwa kama onyo kuwa je, China na Marekani zinapaswa kufuata mwelekeo sahihi wa kusonga mbele kwa utulivu au kurudi nyuma? Aliongeza kuwa uhusiano wa China na Marekani unaanza kuwa imara hivi karibuni, lakini bado unajaribiwa na vitendo hasi.

Alisisitiza kwamba nchi zote mbili zinaweza kujihusisha katika ushirikiano au makabiliano, lakini pia zinaweza kuingia kwenye mizozo.

Aliweka wazi kuwa China inafahamu mipaka yake kuhusu mamlaka, usalama na maendeleo yake na kuionya Marekani kutoivuka.

“Mambo hasi katika uhusiano wetu bado yanaongezeka na uhusiano huo unakabiliwa na kila aina ya usumbufu,” alisema Waziri Wang.

Alieleza kwamba haki halali za maendeleo ya China zimekandamizwa bila sababu na maslahi ya nchi hiyo ya msingi yanakabiliwa na changamoto.

Waziri huyo hakutaja changamoto hizo, lakini kuna mambo kadhaa nyeti kati ya mataifa hayo mawili yenye nguvu yanavutana, ikiwa ni pamoja na misimamo yao kuhusu bahari ya kusini ya China, uungaji mkono wa Marekani kwa serikali ya Taiwan na haki za binadamu.

Waziri Blinken, ambaye yuko katika ziara yake ya pili nchini humo katika muda wa chini ya mwaka mmoja, alikuwa mwangalifu zaidi katika matamshi yake mbele ya waandishi wa habari.

Alisema China na Marekani zina jukumu la pamoja la kuendeleza uhusiano na kujenga diplomasia hai.

Hata hivyo, alisema atakuwa wazi kuhusu tofauti za nchi zao ili kuepuka maneno potofu katika kile alichokiita uhusiano wenye athari kubwa zaidi duniani.

**BBC**

# Serikali yatetea msimamo wake kuhamisha watu Ngorongoro

**Na Frank Monyo**

KATIBU Mtendaji wa Tume ya Taifa ya UNESCO, Prof. Hamisi Malebo, amesema serikali inatekeleza uhamaji wa hiari wa wananchi kutoka Mamlaka ya Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCA) mkoani Arusha ili kulinda haki za binadamu na uhifadhi.

Aliyasema hayo juzi katika mkutano wa kikao cha 23 cha Jukwaa la kudumu la Umoja wa Mataifa la Masuala ya Watu wa Asili (UNPFII) kilichoanza Aprili 15, 2024 jijini New York nchini Marekani.

Prof. Malebo ambaye ameongoza ujumbe wa Tanzania katika kikao hicho, alisema kuwa serikali ya Tanzania ilifanya mapitio shirikishi ya hali ya maisha ya wananchi na uhifadhi katika Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro (NCA) na kubaini umuhimu wa kuweka uwiano sawa wa uhifadhi wa maliasili na utamaduni, maendeleo ya jamii na maendeleo ya utalii.

Alisema ni wazi kwamba, wananchi wanaoishi katika NCA wameathiriwa na migogoro ya binadamu na wanyamapori, magonjwa ya wanyamapori, kukosa haki ya kuwa na makazi ya kudumu, kudorora kwa maendeleo ya kijamii na kiuchumi, kukosa maji safi na salama, na umiliki wa ardhi.

Aliongeza kuwa kutambua haki za binadamu, ambazo zimekuwa sauti ya wanaharakati na wahifadhi mbalimbali na kwa kuzingatia masharti ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania na matakwa ya ulinzi na uhifadhi wa Mkataba wa Urithi wa Dunia wa 1972 na sheria za nchi yaliongoza utekelezaji huo.

Pia alitoa mfano; katika kipindi cha 2018 hadi 2023, watu 65 waliuawa na 205 walijeruhiwa na wanyama pori kama vile simba, chui, fisi, viboko, nyati na tembo.

Alisema wananchi walio katika NCA wanaachwa nyuma katika Malengo ya Maendeleo Endelevu (SDGs).

Prof. Malebo alisema kwa kufuata misingi ya haki za binadamu, serikali imefanya mashauriano na jamii ya wakazi wa Ngorongoro katika kipindi cha miaka 32, ili kwa pamoja kupata ufumbuzi wa kudumu wa changamoto za kijamii na kiuchumi zinazowakabili wananchi wake wanaoishi katika ardhi ya hifadhi.

Alisema mikutano ya uhamasishaji imefanyika kuanzia ngazi ya chini hadi ngazi ya tawala za wilaya na mikoa, wakazi wanaoishi katika NCA ambalo ni eneo lililohifadhiwa, wamepewa elimu kuhusu sheria zinazosimamia utendakazi wa hifadhi ambazo haziruhusu wala kutoa kibali chochote cha kisheria kwa ajili ya shughuli za kijamii na kiuchumi wala kutoa haki ya umiliki wa ardhi katika eneo hilo la hifadhi ambalo pia ni eneo la Urithi wa Dunia.

Alisema wakazi hao walifahamishwa kuhusu manufaa yanayohusiana na kuhama kwao kwa hiari Kwenda katika maeneo yaliyo nje ya hifadhi nchini Tanzania.

Akifafanua juu ya mkakati wa kuhama kwa hiari, Prof. Malebo alibainisha kuwa kwa kuongozwa na Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania, Mikataba ya Umoja wa Mataifa, Tamko la Kimataifa la Haki za Binadamu, Mikataba ya Kimataifa ya Haki za Binadamu, maazimio ya vyombo vingine muhimu vya haki za binadamu na Azimio la Vienna, Serikali ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania inaunga mkono uhamaji wa hiari wa wananchi kutoka Hifadhi ya Eneo la Ngorongoro.

Aliongeza kuwa serikali pia inawezesha zoezi hilo na inabeba gharama za uhamaji, fidia na inatoa mkono wa shukrani kwa wananchi wanaohama kwa hiari Kwenda nje ya eneo la hifadhi.

Serikali inahakikisha wanajamii wanaoishi katika ardhi iliyohifadhiwa wanasaidiwa kuhama na kwenda kuishi katika maeneo ambayo wataendelea na kutekeleza tamaduni zao kwa uhuru tofauti na ambako kwa sasa wanaishi kwa kukabiliwa na changamoto zinazotishia maisha, utamaduni na kuchochea umasikini.

Prof. Malebo pia aliueleza mkutano huo kuwa, serikali imepanga kwa umakini uhamaji wa hiari wa wananchi kutoka katika Hifadhi ya Ngorongoro ambayo ni hatarishi kutokana na ugumu wa maisha na migogoro na wanyamapori jambo ambalo linatoa fursa kubwa za kupunguza maafa na kukabiliana na mabadiliko ya tabianchi kwa wakazi na eneo hilo la Urithi wa Dunia.

"Serikali iliainisha maeneo nje ya hifadhi ambapo wakazi wa Ngorongoro wataweza kuhamia kwa hiari na kuendelea na shughuli zao za kujitafutia riziki kwa amani kama ilivyoainishwa kwenye Katiba ikiwa ni pamoja na kumiliki ardhi na kufanya shughuli za kijamii na kiuchumi,"alisema.



Naibu Waziri Ofisi ya Makamu wa Rais (Muungano na Mazingira) , Khamis Hamza Khamis (wapili kushoto) na viongozi wengine wakishiriki Sherehe za Miaka 60 ya Muungano zilizofanyika jana katika Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam. **PICHA: OMR**

# Mbaroni kwa uhalifu wa baruti, pombe feki, bangi

**Na Gideon Mwakanosya,** SONGEA

Jeshi la Polisi Mkoani Ruvuma linawashikilia watu 29 katika matukio tofauti, likiwemo la kukutwa na dazani 90 za milipuko ikiwemo mbili za milipuko ya baruti kinyume cha sheria.

Akizungumza na waandishi wa habari juzi ofisini kwake, Kamanda wa Polisi Mkoani Ruvuma, Marco Chilya, alisema kutokana na operesheni zinazoendelea mkoani hapa, Aprili 19, mwaka huu, katika Mtaa wa Hoahoa, askari wakiwa kwenye doria, walimkamata Edmund Komba akiwa na dazani mbili za milipuko hiyo.

Aidha, alisema Aprili 20, mwaka huu, katika kijiji cha Nambecha, wilayani Namtumbo, askari polisi wakiwa kwenye doria walimkamata kmtuhumiwa mmoja kwa kosa la kulima bangi ekari mbili na nusu akiwa amechanganya na mazao ya soya, tumbaku, mpunga na maharage.

Kamanda huyo alisema katika upekuzi polisi walikuta bangi kavu kilo 40 iliyofichwa vichakani kwa ajili ya kusafirishwa kwenda nje ya Mkoa wa Ruvuma.

Aidha, alisema katika kijiji cha Njalamatata, wilayani Namtumbo, polisi walimkamata Joseph Kifaru mkazi wa kijiji cha Njalamatata akiwa amelima bangi katika shamba lenye ukubwa wa robo heka likiwa na jumla ya miche 165 ya bangi.

Alisema katika kijiji cha Njalamatata wilayani Namtumbo walimkamata mtu mmoja akiwa amelima ekari moja yenye jumla ya miche 253 ikiwa imezungukwa na mahindi.

Kamanda Chilya alisema Aprili 19, mwaka huu, katika Kata ya Ndongozi waliwakamata watuhumiwa watatu kwa tuhuma za kulima bangi kwenye eneo lenye ukubwa wa ekari moja na kuuza huku wakiwa na kilo sita za bangi kavu.

Alisema baada ya kukamatwa walitaka kuwapa askari rushwa ya Sh. 600,000 lakini walikataa na kuwakamata

Aidha, alisema polisi kwa kushirikiana na Mamlaka ya Mapato Tanzania (TRA), walikamata wafanyabiashara watano kwa tuhuma za kujihusisha na biashara ya pombe feki.

# Zaungana kuendeleza sekta kilimo

**Na Maulid Mmbaga**

BENKI ya Maendeleo ya Kilimo (TADB), imeingia ubia wa miaka mitatu na Airtel Tanzania kwa lengo la kuongeza tija katika sekta ya kilimo kwa njia ya kidijitali kwa kushirikiana na wakulima wakubwa na wadogo na wajasiriamali mbalimbali nchini.

Serikali ilianzisha benki ya TADB kuwakwamua wakulima kwa kuwapatia ruzuku na mikopo ya masharti nafuu, ili kufanya kilimo chenye tija kitakachowasaidia kupiga hatua.

Akizungumza wakati wa hafla ya utiaji saini makubaliano hayo, juzi mkoani Dar es Salaam, Mkurugenzi Mtendaji wa TADB, Frank Nyabundege, alisema ushirikiano huo una dhamira ya kufanikisha kupanua ushirikiano wa sekta ya kifedha kwa wadau mbalimbali, wakiwamo wakulima, wajasiriamali wadogo vijijini, hasa wanawake na vijana.

"Ushirikiano wa Airtel na TADB utafungua milango ya fursa katika sekta ya kilimo na utatoa uwanja mpana kwa wakulima kujipatia masuluhisho kwenye mahitaji na changamoto wanazokutana nazo katika shughuli zao za kila siku. Pia ni mwanzo wa mabadiliko makubwa yatakayowagusa wakulima wote nchini Tanzania," alisema Nyabundege.

Aliongeza kuwa ushirikiano huo unakwenda sambamba na mikakati ya serikali ya kuunga mkono juhudi za wadau wa kilimo kwa kupambana na changamoto mbalimbali ndani ya sekta ya kilimo kwa kuwawezesha wakulima kifedha kama ilivyotajwa na Rais Samia Suluhu Hassan wakati wa mkutano wa wadau wa COP28 mwaka 2023.

"Tunatakiwa kubadilika na kufanya kilimo endelevu kwa kuunga mkono ubunifu mbalimbali unaoendana na hali ya sasa," alisema Nyabundege.

Mkurugenzi Mtendaji wa Airtel Tanzania, Dinesh Balsingh, alisema hatua hiyo ni moja kati ya juhudi za Airtel Tanzania kuunga mkono serikali katika kuleta matokeo chanya katika maisha ya Watanzania, na kwamba wanadhamira ya dhati ya kusaidia jamii kupitia ubunifu katika sekta ya mawasiliano

"Hii ni kwakua tunaamini wakulima wanastahili kuwa miongoni mwa vikundi vinavyotakiwa kunufaika na ukuaji wa teknolojia nchini. Hivyo, ushirikiano wetu na TADB unalenga katika kutatua changamoto zinazowakabili wakulima kwa kutumia bidhaa mbalimbali za kidijitali ambazo zitaibua masoko mapya kwa wakulima mijini na vijijini.

"Bidhaa hizo zitawezesha uzalishaji wa wakulima na kuongeza mapato yao. Na hii ni kutokana na jinsi kilimo kilivyo muhimu katika kuchangia ukuaji wa uchumi wa nchi kwa kuwa zaidi ya asilimia 70 ya watu wamejiajiri katika sekta hiyo," alisema.

# HADITHI

TAARIFA ya Jeshi la Polisi inatangaza kuokotwa kwa maiti ya msichana mzuri na mrembo mno Mariamu, maeneo ya Tabata pembezoni mwa barabara mapema alfajiri. Alikuwa amevalia mavazi ya michezo. Alionekana alikuwa anakimbia, ametoka au anakwenda jogging. Taarifa ya madaktari inasema alikufa kwa mshtuko wa moyo, hiyo inaonyesha kuwa alianguka wakati anafanya zoezi alfajiri ile. Ndugu wa marehemu walikataa ripoti, kwani inaonekana kama alipigwa na kitu kizito kilichonasibishwa na chuma kichwani, kilichosababisha kuwa na tundu kichwani. Ndugu wanaliomba Jeshi la Polisi kufanya uchunguzi wa kina ili kugundua ukweli na wanaapa kuwa kama halikufanyika hilo, damu ya ndugu yao haitoenda bure. Kwani kuna nini? Kila nakala yako ya gazeti la Nipashe, itakupeleka kwenye ukweli wa jambo hili.

# Damu ya Mariamu-10

**Na Adam Fungamwango (0716 350534)**

Kamal alimzoea zaidi Teddy kuliko ndugu wengine. “Yaani mmefanana na dada yako kama korosho.” Kamal alikuwa akimtania Teddy.

“Ikitokea bahati mbaya nikifa, muoe Teddy, mimi nitakuwa radhi kabisa, lakini ukiona mwanamke mwingine nitakutokea usiku wewe na huyo mkeo.” Ni maneno aliyokuwa akiyaongea Mariamu mara kwa mara, anapokuwa na Kamal pamoja na Teddy.

Hakuna aliyekuwa akiyatilia maanani kwa sababu yalionekana ni kama maneno ya utani na kunogesha stori.

“Dada aliyekwambia wewe utaanza kufa kabla ya mimi nani? Ushaanza hivyo, hapa tuko kwenye furaha unaanza mambo yako.” Teddy huwa wanajibu.

“Nasema ikitokea, sisi binadamu, huoni tulivyofanana, Kamal akiwa na wewe ataona kama yupo na mimi tu.”

“Teddy, achana na dada yako, anatuvuruga tu hapa, ukiolewa je, halafu ikitokea yeye amekufa na wewe upo kwenye ndoa, nitaachanisha ili nimuoe?”

Hayo ni maongezi ya mara kwa mara ambayo huongelewa pale, Kamal anapokuwa pamoja na ndugu hao wawili, Mariamu na Teddy, ambapo huwachukua na kwenda nao kula bata, mwenyewe anawaita wake zake, Mariamu mkubwa, Teddy mdogo.

Aliipiga ile namba ili kusikiliza anachotaka kumwambia au anachohitaji. Akapokewa.

“Habari yako shemeji.” Aliisikia sauti ya Teddy ikianza kumsalimia huku ikionekana ina mazingira ya woga hivi.

“Nzuri, vipi tena mke?” Akauliza na kuendeleza utani wao wa kawaida.

“Kwani wewe hujasikia?”

“Nini?”

“Unasakwa na polisi!”

“Unasemaje?”

“Unasakwa na polisi!” Teddy akamwambia tena.

“Kwa kosa gani?”

“Unatuhumiwa kuwa wewe ndiye uliyemuua dada!” Jibu hilo lilimshtua mno Kamal.

“He! Ndiyo yamekuwa hayo eee?”

“Ndiyo shemeji, mimi nimekupigia simu kukutaka ukimbie usikamatwe!”

“Kwa nini nikimbie Teddy wakati mimi sikumuua Mariamu?”

“Sisi tumeambiwa na Jeshi la Polisi baada ya kufanya uchunguzi kwa mara ya pili kuwa wewe ndiyo umehusika, na ushahidi wameutoa!”

“Wewe unaamini kweli kuwa nimemuua Mariamu?”




**“Sawa shemeji.” Akakubali. Kamal akamtajia vitu ambavyo alivihitaji aende kuvichukua nyumbani kwake asubuhi na kumpelekea watakapokutana.**

“Mhh, mimi sijaamini, na ni mimi tu kwenye kikao cha ndugu niliyekuwa nabisha kuwa huwezi kuhusika, lakini nikajua juu, nikaambia mimi na wewe tuna ajenda yetu ya siri, sijui wewe ndiyo unataka kunichukua mimi baada ya kifo cha dada ndiyo maana nakutetea, nikaona aka, ya nini ngoja ninyamaze, maana wanaweza kuongezea kusema tumeshirikiana kumuua dada ili unichukue.”

“Enhe sasa inakuwaje Teddy?”

“Nakusihi shemeji yangu, kimbie, nenda kokote kule, hata nyumbani kwako usirudi, maana leo wametoa taarifa hiyo, ina maana watakuwa wanakuvizia.”

“Mimi sikimbii kwa sababu sijamuua dada yako.”

“Ondoka Kamal, ondoka, kama kuna vitu vya muhimu vipo nyumbani kwako, nitume mimi nitaenda kuvichukua kesho tuonane sehemu uvichukue.”

Kamal alikuwa na wazo kama la Teddy, lakini hakutaka kumwambia moja kwa moja.

Kwa bahati nzuri, ni msomaji mzuri wa vitabu vya riwaya, na mtazamaji wa filamu za kipelelezi, hivyo pamoja na kwamba ni mpenzi wa kuangalia aliiba baadhi ya mbinu za kiitelejensia, upelelezi, pamoja na mambo ya kuzingatia wakati wa kupeleleza jambo, au kujificha ili usikamatwe na wahalifu, wauaji, au watu wengine wabaya.

Kwanza aliamini ni kweli anatafutwa na sababu alitazama kwenye simu yake ya janja ambayo ilionyesha kwenye taarifa za habari za mitandaoni.

Pili alijua, kwa sababu wao polisi ndiyo wanamtuhumu, basi moja kwa moja watamkamata na kumuweka ndani na atafikishwa mahakamani, kila kitu kitakuwa kimeishia hapo.

“Sasa ni hivi Teddy, kesho saa 8:00 mchana tuonane Magomeni Usalama, unasikia?”

“Sawa shemeji.” Akakubali. Kamal akamtajia vitu ambavyo alivihitaji aende kuvichukua nyumbani kwake asubuhi na kumpelekea watakapokutana.

Hakuna mjinga kiasi hicho. Pamoja na kwamba alimwambia shemeji yake kuwa haoni kosa lake, hivyo haoni sababu ya kujificha au kukimbia, ilikuwa ni mdomoni tu si halisi.

Alijua kwa sababu ni Polisi wenyewe ndiyo waliofanya uchunguzi na kugundua kuwa yeye ndiye muuaji, basi angekamatwa na kuwekwa ndani. Asingefanya kitu chochote ili kusaidia kumsaka waliomuua mpenzi wake.

Kila akiisikia ripoti ile ya uchunguzi wa pili, aliishia kutabasamu. Hakutabasamu kwa furaha ila ni mshangao uliochanganyikana na hasira.

Alijua kabisa kuna watu walimchezea ‘picha’ kwa makusudi. Hakumuua mpenzi wake kama inavyosemekana, ila uchunguzi huo umeunganisha matukio ya mawasiliano yake na mpenzi wake dakika za mwisho kabla ya mawasiliano kukatika, ndiyo wakaamua kufanya hivyo.

“Kwa nini mwanzo walisema amekutwa amekufa kwenye mtaro na kuwaambia watu kuwa alianguka akiwa anafanya mazoezi? Kwa nini alivaa nguo za mazoezi? Nani alimvisha hizo nguo? Waliivisha maiti yake au akiwa hai na baadaye kumuua?” Akajiuliza.

Kingine alichojiuliza ni kwa nini uchunguzi wa mwanzo wa madaktari useme kuwa tundu lililopo kichwani lilitokana na kuanguka baada ya kupata mshtuko wa moyo?

“Baada ya ndugu kuchachamaa, kwa nini uchunguzi wa pili ufanyike haraka na kukubali kuwa aliawa na si tena alianguka kwa kupata mshtuko wa moyo na kuanguka kwenye mtaro? Na kwa nini muuaji awe yeye wakati hajafanya kitendo hicho?” Akazidi kuwaza na kujiuliza.

Hii ilimpa picha kuwa yoyote aliye nyuma ya mpango huu atakuwa ni mtu ambaye hapaswi kuangalia kwa jicho jepesi. Ni mtu au watu waliojipanga, wenye uwezo mkubwa wa ushawishi, kwani wameweza hata kuingilia uchunguzi wa kidaktari, pamoja na wa polisi.

Kwa hili hata yeye mwenyewe alijiambia anapaswa kuwa makini, kwani licha ya kusakwa na polisi kwa ajili ya tuhuma hizi, lakini walio nyuma ya mpango huu wanaweza kumsaka na kumuua ili kupoteza kabisa ushaidi.

Kilichomuuma zaidi Kamal ni kuona maadui zake hao ambao hawajui wameweza kumfanya kuwa mbaya kwa jamii na ndugu za marehemu Mariamu, isipokuwa Teddy ambaye hata ukimuwekea bomu mdomoni hawezi kukubali kuwa mauaji na dada yake yamefanywa na yeye.

Alichokuwa anasubiri sasa ni kukutana na Teddy, wakati anamkabidhi vitu vyake muhimu alivyomuagiza amwambie ukweli aliokuwa nao na akitoka hapo aende kuwa balozi kwa ndugu zake kuwaaminisha kuwa hajafanya kitendo hicho. “Sijamuua mpenzi wangu. Siwezi kumuua Mariamu wangu.” Akaongea kwa sauti bila kujijua.

Akaamua kwenda kulala kwenye gesti za bei ndogo mitaa yake Mwanyamala kwa Kopa, ambako alijua si rahisi kwa askari kufanya msako ili kupitisha siku kabla ya kuonana na Teddy.

**Itaendelea Jumamosi**

# MGUNDA AWATAKA SIMBA QUEENS KUIFIKIRIA JKT

**Na Saada Akida**

BAADA ya kufanikiwa kupata ushindi dhidi ya Yanga Princess, Kocha Mkuu wa Simba Queens, Juma Mgunda amewataka wachezaji wake kusahau ushindi huo na kufikiria zaidi mechi iliyopo mbele yao dhidi ya JKT Queens.

Simba Queens juzi ilifanikiwa kuibuka na ushindi wa mabao 3-1 dhidi ya Yanga Princess katika uwanja wa Azam Complex Chamazi Dar es Salaam, ushindi ambao uliwafanya Wekundu hao wa Msimbazi kuongoza msimamo wa Ligi Kuu ya Wanawake.

Baada ya mchezo huo, Mgunda alisema malengo yao ni kuona wanarejesha heshima ya Simba Queens kwa kushinda kila mechi iliyopo mbele yao.

Alisema anatambua ni furaha ya kila Mwanasimba kumfunga mtani wao, lakini sasa wanatakiwa kusahau hiyo mechi hiyo na kuifikiria mechi ijayo dhidi ya JKT Queens ambayo itaamua ubingwa wao.

"Ilikuwa mechi nzuri, Yanga Princess walicheza vizuri na tulipokwenda mapumziko niliwaeleza wachezaji wangu tunatakiwa kubadilika na tulifanikiwa kuwafunga," alisema Mgunda.

Aliongeza kuwa JKT Queens ni wapinzani wao wakubwa na wanatakiwa kuwa makini katika maandalizi kwa sababu mchezo huo utaonesha taswira ya ubingwa wa msimu huu.



Mshindi wa promosheni ya Soka la Afrika limeitika, Raphael Songalaeli (wa pili kulia) akipokea mfano wa hundi ya Shilingi milioni 10 kutoka kwa Meneja wa Tigo mkoa wa Shinyanga, Sadock Phares, wakati wa hafla ya makabidhiano iliyofanyika nyumbani kwa mshindi mtaa wa Mwadui mjini Shinyanga, katikati ni Mwenyekiti wa Mtaa huo Nuru Juma, kushoto ni Mtaalam wa huduma za ziada wa tigo Sostenes Raphael na Meneja Masoko wa kanda ya Ziwa wa Tigo Mussa Mwakapala(kulia) wakipiga makofi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

## Biashara United haijakata tamaa kurejea Ligi Kuu

**Na Adam Fungamwango**

KLABU ya Biashara United imesema licha ya kwamba inaonekana imepoteza nafasi ya kupanda moja kwa moja Ligi Kuu Tanzania Bara, lakini haijakata tamaa kwani inawezekana ikapata nafasi hiyo kupitia mechi za mchujo.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Aman Josiah amesema timu yake bado haijapoteza lengo kwani imekuwa na msimu bora licha ya kupoteza baadhi ya mechi za Ligi ya Championship, ambazo zimesababisha kupoteza nafasi ya kupanda moja kwa moja.

„Lengo letu bado lipo pale pale, kupanda Ligi Kuu, tunajua tayari Kengold imeshapanda Ligi Kuu, lakini pia Pamba ina nafasi kubwa ya kupanda kama ikishinda tu mechi yake ya mwisho, sisi tunasubiri labda iteleze, kitu ambacho naona haitokuwa rahisi sana, ila kwa sasa nguvu zetu tumezielekeza kwenye mechi mbili za mchujo na inavyoonekana tutacheza na Mbeya Kwanza, tukiwatoa tutabaki na mechi zingine mbili kutoka timu ya Ligi Kuu, na hii sasa ndiyo njia yetu ya kuelekea huko na tumejipanga hivyo," alisema kocha huyo.

Biashara United iliyoshuka daraja kutoka Ligi Kuu msimu wa 2021/22, inashika nafasi ya nne ya msimamo wa Ligi ya Championship, ikiwa na pointi 59, ikiwa imepoteza nafasi ya kupanda moja kwa mara, badala yake kusubiri mechi za mchujo.

Matumaini kwa timu hiyo yalifutika mapema wiki hii baada ya kufungwa 2-1 ugenini na Pan African, na hivyo kusalia na pointi zake hiyo, na kuipa mwanya Pamba FC, ambayo ikishinda mechi yake ya mwisho dhidi ya Mbuni FC, itakayochezwa Jumapili kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid, itakuwa timu ya pili kupanda baada ya KenGold.

## JKT yapanga kuimaliza Mtibwa Sugar

**Na Shufaa Lyimo**

KOCHA Mkuu wa timu ya JKT Tanzania, Malale Hamsini amesema baada ya kutoka suluhu na Yanga anaendelea kuimarisha safu yake ya ulinzi kuelekea mchezo ujao na Mtibwa Sugar utakaopigwa Aprili 29 mwaka huu.

Akizungumza na Nipashe jana, alisema atahakikisha safu hiyo inakuwa imara ili asipoteze mchezo huo.

„Ninaendelea kuinoa safu yangu ya ulinzi ili niweze kupata matokeo mazuri katika mchezo huo na lengo ni kushika nafasi ya juu katika msimamo wa Ligi Kuu Tanzania Bara.

Alisema baada ya kumaliza mchezo wao huo uliopita timu iliendelea na kambi na kudai mpaka sasa hana mchezaji yeyote aliyekuwa majeruhi.

Alisema licha ya kuwa Mtibwa Sugar msimu huu haifanyi vizuri kwenye Ligi Kuu anaiheshimu kwa kuwa ni timu yenye uzoefu kwenye Ligi hiyo.

Aliwataka mashabiki wao waendelee kuwaunga mkono na waendelee kuwaamini kwani watapambana kuhakikisha wanapata pointi tatu katika mchezo yao iliyo akiwa msimu huu.

Naye Msemaji wa timu hiyo Masau Bwire alisema wanaendelea kushirikiana na benchi la ufundi ili timu hiyo iendeleze ushindani wake.

## Bingwa wa Chess kutafutwa

**Na Saada Akida**

JUMLA ya washiriki 44 wanachuana kutafuta bingwa wa taifa wa mchezo wa Chess kwa Wanaume na Wanawake kwenye mashindano yanayofanyika kwa siku tatu kuanzia Aprili 26 hadi 28 mwaka huu katika Ukumbi wa Russian Cultural Center, Dar es Salaam.

Kati ya hao Wanaume ni 32 na Wanawake 12 ambao watakwenda kuiwakilisha nchi katika mashindano ya dunia ya Olimpiad yatakayofanyika Septemba huko Budapest nchini Hungary ambapo Tanzania itawakilishwa na washiriki 10.

Haya ni mashindano ya kwanza kufanyika mwaka huu ambapo yatakuwa yakifanyika kwa awamu mbili asubuhi na jioni.

Akizungumza na Nipashe jana, Ofisa Habari wa Tanzania Chess Association (TACA), Mussa Mangula alisema mashindano haya ni muhimu kwani ndio yanaenda kumleta bingwa mpya wa taifa kwa upande wa Wanaume na Wanawake.

„Tunaenda kupata bingwa mpya wa nchi, lakini pia kupata washiriki ambao wataenda kuiwakilisha nchi kwenye mashindano ya kimataifa ya Chess duniani Olimpiad ambayo yatafanyika Budapest, Hungary," alisema Mangula.

„Haya ndio mashindano makubwa zaidi kwa nchi yetu tumepata mwitikio mzuri kutoka kwa wachezaji waliojitokeza isipokuwa tungependa kuwa wachezaji zaidi ya tulionao hivi sasa nafikiri kuna wengine wanaogopa," alisema.

Alisema anapenda kutoa wito wake kwa wanawake wa kitanzania kujitokeza kwa wingi kushiriki mashindano yao kwani kushiriki kwao wanapata uzoefu, wanapata uzoefu na kujifunza mbinu mpya zaidi.

## HABARI MICHEZO

### ZISIKUPITE

**OLISE KUTUA MAN UNITED**
WINGA wa Crystal Palace Mfaransa Michael Olise mwenye umri wa miaka 22, atakuwa tayari kuhamia Manchester United msimu ujao.(***90min***)

**BRANTHWAITE AWANIWA MAN**
MANCHESTER United wana imani dau la kati ya pauni milioni 60 litatosha kumsajili beki wa England, Jarrad Branthwaite mwenye umri wa miaka 21, kabla ya Juni 30. (***Football Insider***)

**GUIMARAES KUUZWA**
ARSENAL na Manchester City zimefahamishwa kuwa Newcastle United wako tayari kusikiliza ofa inayozidi thamani ya pauni milioni 80 kwa kiungo wa kati wa Brazil, Bruno Guimaraes mwenye umri wa miaka 26, msimu huu ujao. (***90min***)

**GUTIERREZ ASAKWA**
KLABU ya Manchester United inaweza kuanza kusaka usajili wa beki wa kushoto wa Hispania, Miguel Gutierrez mwenye umri wa miaka 22 kutoka Girona, lakini wanakabiliwa na ushindani kutoka kwa Arsenal na West Ham. (***GiveMeSport***)

**MIGUEL MIL 100**
KIFUNGU cha kutolewa cha Miguel Guimaraes cha pauni milioni 100 kitaanza kutumika kwa mwezi mmoja pekee, kuanzia mwishoni mwa Mei hadi mwishoni mwa Juni. (***Fabrizio Romano, via Caught Offside***)

**ARSENAL YATAKA WENGI**
KLABU ya Arsenal inafuatilia wachezaji wengi wanaolengwa katika safu ya kati huku kukiwa na wasiwasi kwamba mkataba wa kiungo wa kati wa Real Sociedad na Hispania, Martin Zubimendi mwenye umri wa miaka 25, unaweza kuwa mgumu kufikiwa.(***Standard***)

**MARTIAL KUTEMWA**
KLABU ya Manchester United itamlenga beki mpya wa kati, kiungo wa kati na mshambuliaji katika dirisha la usajili la majira ya kiangazi, huku mshambuliaji wa Ufaransa Anthony Martial mwenye umri wa miaka 28, akiwa miongoni mwa wachezaji ambao hawapo tena katika mipango ya klabu hiyo. (***Football Insider***)

**O'NEIL KUSAINI**
KOCHA wa Wolves, Gary O'Neil huenda akasaini mkataba mpya huko Molineux licha ya ripoti zinazomhusisha na kazi ya Liverpool. (***GiveMeSport***)

**POTTER AWINDWA**
AJAX wana nia ya kumteua kocha wa zamani wa Chelsea na Brighton, Graham Potter ambaye pia yuko kwenye orodha ya Manchester United ya watu wanaoweza kuchukua nafasi ya Erik ten Hag. (***Guardian***)

**LUNIN AGOMBEWA**
KLABU za Manchester United, Paris St-Germain na Bayern Munich zote zinavutiwa na mlinda mlango wa Real Madrid raia wa Ukraine, Andriy Lunin mwemye umri wa miaka 25. (***Fichajes***)

**SOLSKJAER ATAJWA CANADA**
KOCHA wa zamani wa Manchester United, Ole Gunnar Solskjaer na mkufunzi wa zamani wa Leeds United, Jesse Marsch wamewasiliana na Canada kuhusu kuiongoza timu ya taifa katika Kombe la Dunia la 2026. (***Standard***)

# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA




# FERNANDEZ KUFANYIWA UPASUAJI

## Hataichezea Chelsea kwa kipindi cha msimu kilichobaki pia...

**MANCHESTER,** England

KIUNGO wa kati wa Chelsea, Enzo Fernandez anatarajiwa kufanyiwa upasuaji wa henia ambapo utamfanya kuwa nje ya uwanja kwa kwa muda mrefu na amehitimisha msimu wake huu.

Mchezaji huyo wa kimataifa wa Argentina amekuwa akipambana na tatizo hilo kwa wiki kadhaa sasa na hivi karibuni alikosa mchezo wa ushindi wa mabao 6-0 dhidi ya Everton huku akiendelea kujaribu kudhibiti maumivu.

Hata hivyo, Hernan Castillo sasa amefichua kwamba Fernandez anaweza kupasuliwa huku akitumai kupona kwa wakati ili kuonesha kiwango chake bora kwenye Copa America msimu huu wa joto.

Ole aliongeza kuwa Chelsea imekuwa ikiwasiliana mara kwa mara na maafisa wa afya kutoka timu ya taifa ya Argentina na sasa imekubaliwa kwa kauli moja kwamba Fernandez afanyiwe upasuaji sasa, badala ya kusubiri hadi majira ya joto.

Fernandez anatarajiwa kuhitaji angalau wiki tatu kuwa nje ya uwanja na kuna uwezekano hataichezea tena Chelsea hadi mwisho wa msimu wa Ligi Kuu, huku Chelsea ikitarajiwa kumenyana na Bournemouth siku ya mwisho ya kampeni Mei 19.

Mashabiki wengi wametaja jeraha la Fernandez kama sababu inayowezekana ya mwenendo wake duni uwanjani, lakini bosi wa The Blues Mauricio Pochettino anaamini kuwa kiungo huyo anapambana na kipindi cha kawaida cha marekebisho katika klabu yake mpya.

"Kwa Enzo, baada ya Kombe la Dunia kufika hapa, katika timu ambayo haikuwa thabiti, ngumu kupata matokeo chanya, kila mara ilikuwa ngumu sana," alisema Pochettino.

**"Katika majira ya joto alihusika katika michezo mingi na alifika mwishoni mwa msimu, hajapata likizo katika miaka miwili iliyo pita.**

"Mambo mengi hasi yalitokea. Ilikuwa vigumu kwake yeye na familia yake kuzoea mazingira. Si rahisi kuzoea na kufanya haraka hivyo.

"Kwa hakika atakuwa bora zaidi msimu ujao, baada ya uzoefu wa msimu mzima katika kikosi hiki na timu hii.

"Ni mzoefu zaidi, anapata hisia nzuri zaidi. Msimu mzima ni mzuri kwake kujifunza. Hata kama ni bingwa wa dunia, anahitaji kuzoea Ligi Kuu na klabu hii. Kwangu mimi sina shaka kwamba atakuwa bora zaidi."

# WAKALA WA BEN AWAKOSOA WAKOSOAJI

**LONDON,** England

WAKALA wa Beki wa Arsenal, Ben White, amewataka Mashabiki wa soka nchini England kumtendea wema mchezaji wake anapokuwa katika majukumu yake ndani na nje ya Uwanjani.

White aliifungia Arsenal mabao mawili katika ushindi wa mabao 5-0 dhidi ya Chelsea kwenye mchezo wa Ligi ya England, Jumanne Uwanja Emirates jijini London.

Alexander Levack wakala wa beki huyo mwenye umri wa miaka 26, amekiri kuwa muhanga wa shutuma anazozipata mteja wake, hasa baada ya kuchukua uamuzi wake wa kutoichezea England chini ya Kocha Mkuu Gareth Southgate.

Levack amendika katika kurasa zake wa mitandao ya kijamii: "Ninahisi kulazimishwa kuandika hii leo baada ya uwezo mkubwa aliounesha White katika mchezo dhidi ya Chelsea na kufunga mabao mawili.

"Kwa muda wa majuma manne yaliyopita Ben amekuwa kwenye vyombo vya habari na mitandao ya kijamii kwa kiasi kikubwa, lakini kwa asilimia kubwa alitajwa kwa mambo mabaya pekee na wengine wakashiriki kumchafua.

"Ingawa ninashukuru kuwa Ben aliendelea kuwa mpole na kushiriki shughuli zake hadharani, jambo ambalo linaleta maana kwake na kuwaacha midomo wazi wakosoaji, nilitaka kusema kwamba hisia huyu ni binaadamu ambaye ana hisia sawa na sisi sote.

"Ben ameonyesha uimara na nguvu za ajabu katika kipindi hiki kigumu nje ya uwanja na amezuia kelele zote na amefanya vizuri sana uwanjani, katika hali ambayo wengine wengi wasingeweza na wangepotea kabisa.

"Ben ana tabia ya ajabu na amefanya vizuri sana uwanjani, mtazamo ambao unamruhusu kuendelea kuonesha uwezo wa kuzunguka katika maisha yake ya kazi na ya kibinafsi, nadhani ujumbe mkuu ni kuwa mkarimu kwa watu.

"Kwa upande wa Ben hatutaki kusema hadharani, na mimi sitaki kujua nini kinaendelea katika maisha ya kibinafsi ya watu kwa hivyo tafadhali tujaribu kuwa na huruma na kuheshimu maisha ya watu wengine."




# Olise anatamani kuhamia Man U

**MANCHESTER,** England

MICHAEL Olise atakuwa tayari kuhamia Manchester United majira ya kiangazi iwapo Mashetani Wekundu hao wataimarisha nia yao ya kumnunua, vyanzo vimeiambia 90min.

Mchezaji huyo mwenye umri wa miaka 22 amepambana msimu huu na matatizo mbalimbali ya majeraha, lakini amesalia kuwa mmoja wa wachezaji bora wa Crystal Palace kila anapokuwa fiti.




90min hapo awali iliripoti kwamba Olise alikuwa akilengwa na United msimu huu wa joto huku akivutiwa na serikali za zamani na mpya huko Old Trafford kufuatia Sir Jim Ratcliffe na INEOS kuinunua klabu hiyo.

Mashetani Wekundu wanaweza kuhamisha wachezaji kadhaa mwishoni mwa msimu. Mshambulizi Anthony Martial ataondoka mkataba wake utakapomalizika, winga Antony anaweza kuuzwa na mustakabali wa kiungo Christian Eriksen uko hewani, na mchezaji hodari kama Olise atasaidia kufidia pengo la ubunifu la baadhi ya wachezaji au wote walioondoka.

Hata hivyo, licha ya ripoti kupendekeza vinginevyo, vyanzo vimeiambia 90min kwamba Chelsea kwa sasa hawana mpango wa kurejesha nia yao ya Olise na hawashindani na United kwa ajili ya saini yake msimu huu wa joto.

Olise alisaini mkataba mpya na Palace msimu uliopita wa joto baada ya The Eagles kutishia Chelsea kwa hatua za kisheria.

# Arne Slot aiingiza vitani Liverpool

**LIVERPOOL,** England

UONGOZI wa Klabu ya Liverpool utakuwa na upinzani mkali kutoka kwa FC Bayern Munich, katika vita ya kuiwania saini ya Kocha wa Klabu ya Feyenoord ya Uholanzi Arne Slot.

Kocha wa Bayern, Thomas Tuchel ataondoka mwishoni mwa msimu huu 2023/24, baada ya mambo kumuendea vibaya na tayari uongozi umeshafikia makubaliano ya kuachana naye.

Gazeti la The Independent la England limeripoti kuwa Kocha Slot yuko tayari kuanza mazungumzo na Uongozi wa Liverpool.

"Liverpool wamefanya mazungumzo na Feyenoord kwa ajili ya Arne Slot baada ya kumtambua Mholanzi huyo kama mgombea wanayempendekeza kuchukua mikoba ya Jurgen Klopp.

"Slot, ambaye alishinda Kombe la Uholanzi juma lililopita na Eredivisie msimu uliopita, amebakiza miaka miwili katika mkataba wa miaka mitatu aliousaini msimu uliopita.

"Liverpool inaweza kukabiliana na ushindani kwa kocha huyo mwenye umri wa miaka 45 kutoka FC Bayern Munich huku Slot akiibuka kama mshindani wa kazi kadhaa kuu ambazo zitatolewa msimu huu wa joto.

"Liverpool wametathmini wasifu wa makocha mbalimbali, huku Ruben Amorim wa Sporting Lisbon akiwa mstari wa mbele baada ya kuwavutia viongozi wa klabu hiyo, huku chaguo lao la kwanza Xabi Alonso, akikataa kuondoka Bayer Leverkusen."



# LIGI KUU Z'BAR KURINDIMA KESHO

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

LIGI Kuu ya Zanzibar inatarajiwa kuendelea tena Aprili 28 mwaka huu baada ya kusimama kwa muda wa mwezi mmoja na nusu.

Ligi hiyo ambayo wakati inasimama tayari timu zote zilikuwa zimecheza michezo 20 ambapo iliyobaki ni michezo 10 ya kumaliza msimu wa Ligi wa 2023-2024.

Kwa mujibu wa ratiba iliyotolewa na Bodi ya Ligi Zanzibar inaonesha katika kisiwa cha Unguja kutakuwa na mchezo kati ya Zimamoto na Uhamiaji, mchezo ambao utachezwa katika uwanja wa Mao Zedong A siku hiyo ya Aprili 28.

**Aidha mchezo mwingine ambao utachezwa katika uwanja wa Finya kisiwani Pemba utakuwa ni kati ya wakongwe wa soka visiwani hapa timu ya Jamhuri itakayopepetana na Hard Rock.**

Hata hivyo, ratiba hiyo inaonesha siku ya pili ambayo itakuwa ni Jumatatu ya April 29, mwaka huu, pia kutakuwa na michezo miwili, ambapo Manedelo na Chipukizi watacheza uwanja wa Finya na Malindi itacheza na Mlandege Mao Zedong A.

Akizungumza na gazeti hili Mtendaji Kuu wa Bodi ya Ligi Zanzibar, Issa Kassim alisema maandalizi ya kuelekea michezo hiyo ya lala salama imekamilika.

Alisema Bodi ya Ligi kwa kushirikiana na kamati nyingine zinazohusika katika kusimamia Ligi hiyo watakuwa makini hasa katika michezo hii ya kupata Bingwa na timu zinazoshuka daraja.

"Tunataka kuhakikisha hakuna vitendo vyoyote au viashiria vya upangaji wa matokeo katika michezo hii muhimu,"alisema.

Ligi kuu ya Zanzibar wakati inasimama ilikuwa ikiongozwa na timu ya Jeshi la Kujenga Uchumi (JKU), wenye alama 41, wakifuatiwa na mabingwa watetezi wa ligi hiyo KMKM wenye alama 39, wakati Zimamoto ipo nafasi ya tatu alama 37.

Jumla ya timu nne zinatarajiwa kushuka katika ligi hiyo, ambayo inashirikisha timu 16 katika msimu huu.

## Ruvu Shooting yashuka tena daraja

**Na Adam Fungamwango**

TIMU ya Ruvu Shooting imeshuka daraja baada ya kutoka suluhu dhidi ya Transit Camp katika mechi ya Ligi ya Championship katika mechi iliyochezwa Uwanja wa Samora, Iringa.

Timu hiyo sasa itashiriki Ligi Daraja la Pili ‚first league', msimu ujao baada ya kuteremka kutoka Ligi ya Championship, msimu mmoja tu baada ya kushuka kutoka Ligi Kuu Tanzania Bara.

Ruvu Shooting ilishuka daraja kutoka Ligi Kuu, msimu wa uliopita wa 2022/23 na msimu wa kwanza tu kucheza Championship, imeshindwa kuhimili vishindo na sasa imeshuka tena.

Timu hiyo imeshuka kwa kuwa ina pointi 13 mpaka sasa na inashika mkia, ikibakisha mechi moja tu dhidi ya Green Warriors, ambayo hata kama ikishinda itakuwa na pointi 16 ambazo tayari zimeshapitwa na Pam African, yenye pointi 19.

Pan, ambayo ilishinda mabao 2-1 dhidi ya Biashara United wiki hii, ilifikisha idadi hiyo ya pointi na kuhitimisha safari ya Ruvu Shooting.

Hata hivyo, Pan African, Mabingwa wa Tanzania Bara mwaka 1982, haiko salama kwani wanahitaji ushindi katika mechi yao ya mwisho Jumapili ijayo dhidi ya Stand United, Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam.

Timu hiyo yenuye pointi 19, ikishinda itafikisha pointi 22, ambazo zinamilikiwa na Copco inayoshika nafasi ya 14.

Iwapo Copco itatoka sare katika mechi yake ya mwisho dhidi ya TMA kesho, katika mechi inayotarajiwa kuchezwa, Uwanja wa Black Rhino, Karatu, Arusha, Pan African nayo itaungana na Ruvu Shooting kushuka daraja kwenda ‚first league'.



Yusuf Mdoe (kushoto) na Mohammed Lakha wakicheza mchezo wa Chess wa kumtafuta bingwa wa taifa kwa upande wa Wanaume mashindano yaliyofanyika kwenye Ukumbi wa Russian Cultural Center, Dar es Salaam jana. **PICHA MPIGAPICHA WETU**

## *Simba yaivaa Azam fainali*

INATOKA UKURASA 24

Nahodha Msaidizi, Mohamed Hussein ‚Tshabalala', amesema kutokana na maandalizi waliyofanya wanatarajia ushindi.

„Nafikiri kutokana na maandalizi tuliyoyafanya, inatupa mwanga mzuri, naamini tutafanya vizuri, najua Azam ina wachezaji wazoefu kwenye michuano yote, kwa hiyo hakuna mechi nyepesi tukicheza nao, ni kupambana tu," alisema.

Kocha Bruno Ferry, ametabiri mechi kuwa nzuri kutokana na aina ya soka la timu zote mbili na kiwanja kitakachochezwa kuruhusu ‚boli' kutembea.

„Simba ni timu kubwa nchini na ina historia ndefu, hivyo tunajua kuwa tutakuwa na mechi nzuri na ngumu, nafikiri kwa sababu timu zote zinaweka mpira chini, na uwanja ni mzuri, watu watainjoi.

Ila nimewaambia wachezaji wangu kuwa kwa sababu tunacheza na timu kubwa, tunachotakiwa kufanya ni kuwa na umaliziaji mzuri wanapokuwa ndani ya eneo la hatari," alisema kocha huyo.

Mchezaji wa timu hiyo, Lusajo Mwaikenda alisema wachezaji wenzake wako tayari kutoa walichonacho kuhakikisha wanatwaa ubingwa.

„Tupo vizuri, kila mchezaji yupo tayari, sisi tunauona ni mchezo mkubwa, hivyo kila mchezaji atatoa alichonacho, tunautaka ubingwa," alisema.

## Yanga hasira zote kwa Coastal Union leo

INATOKA UK. 24

tunakwenda kucheza na timu iliyokamilika, kwanza pasi zao, mikimbio yao, wanajua kutumia uwanja vyema, pili ni uwezo wa mchezaji mmoja mmoja na hilo ndilo tunakwenda kukabiliana nalo.

Kwa hiyo sisi tumejiandaa kwa sababu tumetafuta mbinu ambazo zitatupa faida kwenye hii mechi, kwa sababu tumeshajua tunacheza na timu ya aina gani," alisema kocha huyo.

Katika mechi ya mzunguko wa kwanza iliyochezwa, Novemba 8 mwaka jana, Uwanja wa Mkwakwani, Tanga, Yanga ilishinda bao 1-0 lililofungwa na Clement Mzize.

Yanga inayoongoza ligi ikishinda itafikisha pointi 62 ambazo zitaifanya kuwa kwenye nafasi nzuri ya kuchukua tena ubingwa.

Coastal Union nayo inahitaji ushindi kwa udi na uvumba ili kujishindia katika nafasi ya nne iliyopo.

Timu hiyo ina pointi 33, na kama ikishinda itafikisha 36 na kuikimbia KMC ambayo inainyemelea nafasi hiyo inayotoa uwakilishi wa nchi kwenye michuano ya kimataifa, iwapo bingwa wa Kombe la FA, atapata moja kati ya nafasi tatu za juu.

Michezo

Jumamosi Aprili 27, 2024

Nipashe



Fernandez kufanyiwa upasuaji UK. 21



Kibu Denis

Fei Toto

# Simba yaivaa Azam fainali ya Muungano bila Chama

## Ni baada ya miaka 20 ya mashindano hayo huku...

**Na Adam Fungamwango**

FAINALI ya Kombe la Muungano inatarajiwa kuchezwa kwa mara ya kwanza leo baada ya miaka 20 kupita, wakati Simba itakapokwaana na Azam FC kwenye Uwanja wa New Amani Complex, mjini Zanzibar.

Simba iliingia fainali kwa kuichapa KVZ mabao 2-0, huku Azam, ikiishindilia KMKM mabao 5-2, mechi zilizochewa kwenye uwanja huo huo.

Itakuwa ni nafasi nzuri ya timu zote kutwaa taji hilo, ambapo kama Simba ikishinda itakuwa imejiwekea kibindoni taji la pili msimu huu, baada ya kutwaa Ngao ya Jamii, Agosti 13 mwaka jana kwenye Uwanja wa Mkwakwani, Tanga ilipowafunga watani zao wa jadi, Yanga kwa mikwaju ya penalti 3-1 na litakuwa taji la kwanza kwa Azam msimu huu.

Katika fainali ya leo, Simba itakuwa na pigo la kumkosa mmoja wa wachezaji wake tegemeo kwa ufungaji na utoaji wa pasi za mwisho, ‚asisti', Clatous Chama, aliyeumia katika mechi iliyopita dhidi ya KVZ.

**Mbali na mchezaji huyo, pia ita wakosa Henock Inonga, ali yeumia katika mechi ya dabi, kati ya timu hiyo dhidi ya Yan ga, iliyochezwa, Aprili 20, na Saido Ntibazonkiza.**

Kocha Msaidizi wa timu hiyo, Selemani Matola, amesema mechi haitokuwa nyepesi, si kutokana na ubora wa Azam tu, bali huwa wakikutana mchezo huwa mgumu.

"Haiwezi kuwa fainali nyepesi, ni ngumu na nzuri kwa sababu zinakutana timu zenye uwezo, ziko vizuri, ukiangalia Azam ina kiwango kikubwa msimu huu.

Katika mechi hii sisi tumejipanga, pamoja na ubora na uzuri wao, tumejiandaa kupambana kupata ushindi katika mechi ya fainali, tutaingia kwa tahadhari na heshima kubwa kwa Azam kwa sababu tukikutana shughuli huwa pevu, ila tunawaahidi mashabiki wetu matokeo mazuri," alisema Matola.

Matola pia aliwataja wachezaji ambao watakosa mchezo wa leo, lakini akawatoa hofu mashabiki wa timu hiyo kuwa waliobaki wako fiti na wameahidi kuipigania nembo ya Simba.

"Tuna majeruhi ambao ni Inonga, Saido, ambao wameanza kurejea taratibu mazoezini, lakini pia katika mechi iliyopita tulizalisha mwingine ambaye ni Clatous Chama ambaye msitarajie kumuona katika mchezo huu, waliosalia wapo tayari na mchezo," alisema.

INAENDELEA UK. 23

# Yanga hasira zote kwa Coastal leo

**Adam Fungamwango na Saada Akida**

BAADA ya kulazimishwa suluhu Jumatano iliyopita dhidi ya JKT Tanzania katika Uwanja wa Meja Jenerali Isamuhyo, Mbweni, Dar es Salaam, Mabingwa Watetezi wa Ligi Kuu Tanzania Bara, Yanga, leo wanatarajia kumalizia hasira zao kwa Coastal Union kwenye Uwanja wa Azam Complex, Chamazi, wakisaka pointi tatu zitakazowaweka katika mazingira mazuri ya kutwaa ubingwa kwa mara ya tatu mfululizo.

Kocha Mkuu wa timu hiyo, Miguel Gamondi, amesema baada ya suluhu hiyo ambayo hawakuitarajia, wana njaa ya ushindi, hivyo wataingia uwanjani kama mbogo aliyejeruhiwa kwa ajili ya kusaka ushindi.

"Tulicheza mechi yetu ya mwisho hali ya hewa ikiwa mbaya, lakini tutaangalia nini kitatokea kesho, najua tutakuwa na mechi ngumu na tutajitahidi kufanya kile kinachotakiwa kufanywa ambacho ni kushinda mechi bila kuangalia nini kimetokea katika mechi iliyopita.

Tuna njaa ya kupata pointi tatu, kwetu ni muhimu, tunajua tunacheza na timu ngumu, inazuia vizuri sana," alisema Gamondi.

Kocha huyo alisema ana uhakika kuwa Coastal Union itakuja na staili ya kupaki basi na kushambulia kwa kustukiza, hivyo amejiandaa na hilo.

"Kuna wakati huwa sipendi sana timu ambazo zinazuia sana kwa sababu mpira ni mchezo wa kuonyeshana ufundi, ustadi wa kushambulia na kutafuta nafasi, lakini zipo timu zina sababu ya kufanya hivyo, hawawezi kupishana, kwa hiyo tunachotakiwa ni kuvunja ngome na kutumia nafasi chache tutakazozipata," alibainisha kocha huyo.

Akizungumzia kuelekea katika mechi ya leo, Kocha Mkuu wa Coastal Union, David Ouma, alisema mechi kwao itakuwa ngumu kwa sababu wanakwenda kucheza na timu iliyokamilika kila idara.

"Tunacheza ugenini na Yanga,

INAENDELEA UK. 23

GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

9 770856 541002 >